# KATIBA YA CHAMA CHA KIJAMII (CCK)

## TOLEO LA APRILI 2013

**Toleo hili la Katiba ya Chama Cha Kijamii (CCK), la Aprili 2013 ni toleo la pili tangu kutungwa kwa katiba hii Julai 2010.**

**Kwa hali hili ni toleo ambalo limezingatia na kuweka pamoja marekebisho na maboresho ya katiba yaliyoandikwa katika toleo la kwanza la CCK Julai 2010.**

## YALIYOMO

YALIYOMO ....................................................................................................................... 1
SURA YA KWANZA ............................................................................................................ 2
UTANGULIZI ........................................................................................................................ 2
1.1 TAMKO RASMI ............................................................................................................. 2
1.2 DIRA NA MWELEKEO WA CHAMA ............................................................................ 3
SURA YA PILI ...................................................................................................................... 4
CHAMA, UANACHAMA NA UONGOZI ............................................................................... 4
2.1 JINA LA CHAMA ............................................................................................................ 4
2.2 ALAMA KUU ZA CHAMA ............................................................................................. 4
2.3 MAKAO MAKUU YA CHAMA ....................................................................................... 4
2.4 IMANI MADHUMUNI MALENGO NA ITIKADI YA CHAMA .......................................... 4
2.5 UANACHAMA NA UONGOZI NDANI YA CHAMA CHA KIJAMII ................................... 5
SURA YA TATU ................................................................................................................... 8
VIKAO VYA CHAMA ............................................................................................................ 8
3.1 VIKAO VYA CCK ............................................................................................................ 8
3.2. NGAZI YA SHINA ........................................................................................................... 8
3.3 NGAZI YA KITONGOJI ................................................................................................. 10
3.4 NGAZI YA TAWI ........................................................................................................... 12
3.5 NGAZI YA KATA ........................................................................................................... 14
3.6 NGAZI YA WILAYA YENYE MAJIMBO YA UCHAGUZI ZAIDI YA MOJA ..................... 16
3.7 NGAZI YA MKOA .......................................................................................................... 18
3.8 NGAZI YA TAIFA ........................................................................................................... 20
SURA YA NNE ..................................................................................................................... 25
UONGOZI WA KITAIFA ....................................................................................................... 25
VIONGOZI WAKUU WA CCK NA WATENDAJI CCK .......................................................... 25
4.1. VIONGOZI WAKUU WA CHAMA ................................................................................... 25
SURA YA TANO .................................................................................................................. 28
WAGOMBEA URAIS NA WAGOMBEA WENZA .................................................................. 28
5.1 WAGOMBEA URAIS NA WAGOMBEA WENZA ............................................................ 28
SURA YA SITA .................................................................................................................... 29
MENGINEYO ....................................................................................................................... 29
6.1 VITENGO VYA CHAMA CHA KIJAMII ............................................................................ 29
6.2 UTARATIBU WA KUCHAGUA WAGOMBEA NAFASI ZA UONGOZI. ............................. 31
6.3MALI NA FEDHA ZA CHAMA ......................................................................................... 31
6.4 NAFASI ZIKIWA WAZI ................................................................................................... 32
6.5 BARAZA LA WADHAMINI .............................................................................................. 32
6.6 MAAMUZI YA VIKAO VYA CCK ..................................................................................... 33
6.7 TAASISI NA NAFASI NYINGINE ZA CCK ....................................................................... 34
6.8 MAREKEBISHO YA KATIBA YA CCK. ............................................................................ 37
6.9 KUVUNJA CHAMA ......................................................................................................... 37

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 TAMKO RASMI

Kwa kuwa mapambano ya kuleta Uhuru wa nchi yetu yaliyoasisiwa na wazee wetu Julius K. Nyerere na Abeid A. Karume yalikuwa na lengo kuu la kumuondoa Mwananchi kutoka kwenye unyonge wa kunyonywa, kunyanyaswa na kudharauliwa na wakoloni, ambao ni ukombozi wa mwananchi kisiasa, kiuchumi na kijamii: na

Kwa kuwa uhuru tulioupata ulitupatia fursa ya kujenga nchi na Taifa lenye kubeba matumaini ya wananchi wote kwa ujumla kwa kuweka misingi imara ya kuheshimu na kuzingatia usawa wa binadamu, uongozi bora uongozi wa sheria. Haki za binadamu hifadhi na ustawi kwa wananchi wote na Utaifa wetu na

Kwa kuwa ukombozi kamili wa mwananchi kisiasa, kiuchumi na kijamii unahitaji viongozi wenye uzalendo, uadirifu, wasio wabinafsi, juhudi, maarifa, moyo wakujituma na ujasiri wa kuthubutu kwa upande wa viongozi sifa ambazo zimefifia kwa sasa hapa nchini

Kwa kuwa nchi yetu imedhamiria kikatiba kuthamini na kuzingatia uhuru wa mahakama katika utoaji haki bila woga wala upendeleo na uhuru wa Bunge lenye madaraka kwa niaba ya wananchi kusimamia na kuishauri serikali na vyombo vyake katika utekelezaji wa shughuli za umma na :

Kwa kuwa Tanzania inao utajiri wa kutosha wa rasilimali unaoweza kuleta maendeleo ya haraka ya nchi kiuchumi na kuleta mabadiliko makubwa ya maisha kwa kila mwananchi ikiwa ombwe la uongozi litashughulikiwa na

Kwa kuwa matumizi bora na endelevu ya utajiri wa rasilimali yanawezekana tu katika Taifa ambalo lina uongozi wenye uchungu na nchi na unaozingatia maadili kama yalivyoainishwa na kusimamiwa kidete na Baba wa Taifa Mwalimu Julius K. Nyerere.Taifa ambalo linawaandaa vijana wake vizuri Kielimu na Kimaadili na ambalo wanawake wanafursa sawa na wanaume na ambalo mchango wa kila raia awe kijana Mzee, Mlemavu n.k. unatambuliwa na kuthaminiwa: na

Kwa kuwa Elimu ni moja ya Misingi ya Maendeleo ya Taifa lolote lile, Msingi ambao Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere aliutumia kujenga Taifa jipya lenye matumaini, nchi yetu haina budi kuendeleza utaratibu wa Serikali kugharamia elimu ya wananchi wake : na

Kwa kuwa adui mkubwa wa haki na maendeleo ni UFISADI yaani rushwa ubadhirifu wa mali ya Umma na uporaji wa rasilimali za Taifa, adui ambaye hana budi kupigwa vita kwa nguvu zetu zote: na

Kwa kuwa Muungano wa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar ni ushahidi hai na tosha unaobeba matumaini mahsusi ya kuziunganisha nchi za Kiafrika kuwa moja katika kukabiliana na changamoto za utandawazi: na

Kwa kuwa Tanzania ni nchi iliyodhamiria kikatiba kufuata mfumo wa demokrasia ya vyama vingi na

Kwa kuwa lengo kuu la mfumo wa demokrasia ya vyama vingi ni kujenga na kuimarisha nguvu za umma na uwezo wa wananchi mmoja mmoja na kwa pamoja katika kubadilisha mazingira ya Nchi yao na maisha wanayoishi : na

Kwa kuwa lengo hili kuu la kuijenga na kuimarisha nguvu za umma na uwezo wa wananchi inawezekana tu ikiwa wananchi wataungana na kuongozwa na Chama cha siasa kilicho madhubuti na chenye matumaini mapya kwao na kisichoyumba kwenye masuala ya msingi, Chama chenye itikadi na sera za kimaendeleo, chama kinachoweka hai matarajio ya wananchi baada ya uhuru wa kiuchumi na kijamii chama kinachopiga vita aina zote za ubaguzi wa kimaumbile kwa kauli na vitendo na pia chama chenye msimamo thabiti wa kujali nchi na watu wake kwanza kabla ya Maslahi mengine yoyote.

HIVYO BASI SISI WANANCHI WAZALENDO tuliokutana hii leo tarehe 20 Julai 2010 Jijini Dar es Salaam kutekeleza wajibu wetu kikatiba wa kuunganisha pamoja mawazo yetu na kuunda Chama cha Siasa kinachozingatia changamoto zote zinazoikabili nchi yetu tangu baada ya Uhuru na kitakachobeba matarajio ya wananchi ya leo na kesho, kwa jina la CHAMA CHA KIJAMI, kwa kifupi CCK ili pia kiweze kutambuliwa kisheri na kiandikishwe kama Chama cha Siasa ambacho lengo lake kuu ni kuleta mageuzi ya Kitaifa kwa kufuata mfumo wa Kidemokrasia, tukijidhatiti kisiasa, kiuchumi katika Jamii ya Watanzania kwa faida yetu sote sasa na vizazi vijavyo.

## 1.2 DIRA NA MWELEKEO WA CHAMA

1.2.1 CCK itahakikisha kwamba inasimamia haki na maslahi kwa makundi yote kama ifuatayo

a. Wakulima na wafugaji
b. Wafanyakazi kwenye sekta zote
c. Wajasiriamali pamoja na vyama vyao kuhusiana na mabadiliko ya kimfumo wa kimaslahi, kufanya hivyo bila ya mitafaruku.

1.2.2. CCK itayaweka bayana matatizo makubwa ya wananchi hasa kuanzia ngazi ya chini yanayowakabili wanajamii hao itaelekeza nguvu zake zote kwa mashirikiano ya pamoja ili kuweza kufikia ufumbuzi wa kero zao kwa kuyatafutia uwezo wa kuyatatua kwa faida ya wanajamii **(kabla ya chama kushika Dola)** kwa usimamizi wa viongozi wa CCK.

## SURA YA PILI

## CHAMA, UANACHAMA NA UONGOZI

### 2.1 JINA LA CHAMA

Jina la chama ni CHAMA CHA KIJAMII
Chama kitatumia herufi CCK kama ufupisho badala ya jina lake kamili.

### 2.2 ALAMA KUU ZA CHAMA

2.2.1 BENDERA

(a) Bendera ya CCK itakuwa na rangi nne yaani Bluu bahari, Nyeupe, Njano na nyeusi
(b) Rangi ya Blue ni kielelezo cha kwamba Tanzania ina eneo kubwa la Bahari, maziwa na mito.
(c) Rangi Nyeupe ni kielelezo cha amani na upendo pamoja na ushirikiano mwema na nchi za nje.
(d) Rangi ya Njano ni kiashirio cha rasilimali kubwa ya madini iliyoko nchini mwetu.
(e) Rangi Nyeusi ni kielelezo cha watu

2.2.2 ALAMA YA CHAMA

(a) CCK Itatumia nembo ya mikono miwili wa mwanaume na mwanamke ambayo itashikana kwa uelekeo wa juu huku maana yake ikiwa ni umoja na mshikamano.
(b) Ufafanuzi
Nembo hii inadhihirisha kuwa jamii ya Watanzania kuwakilishwa na makundi yote yanayopaswa yawe na mshikamano wa dhati kwa kuzingatia mambo makuu muhimu yafuatayo: UPENDO, AMANI, HESHIMA, MSHIKAMANO na MAELEWANO.

### 2.3 MAKAO MAKUU YA CHAMA

2.3.1 Makao makuu ya chama cha CCK yatakuwa jijini Dar es salaam – Tanzania na Ofisi nyingine ndogo za makao makuu zitakuwa Zanzibar na Dodoma.

2.3.2 CCK itaanzia kwenye mashina na itaendesha shughuli zake ilizojiwekea kwa kuzingatia KATIBA, KANUNI na miongozo yake, bila kuathiri Katiba ya Nchi kwa manufaaa ya Jumuiya ya Watanzania.

### 2.4 IMANI MADHUMUNI MALENGO NA ITIKADI YA CHAMA

2.4.1 CCK kinaamini kwamba:-

(1) Binadamu wote huzaliwa huru, na wote ni sawa;

(2) Kila mtu anastahili heshima ya kutambuliwa na kuthaminiwa utu wake;

(3) Hifadhi na ustawi wa jamii yetu vitapatikana kwa matumizi bora na endelevu ya utajiri wa rasilimali tulizonazo, serikali kuwajibika kwa wananchi ambao ni

msingi wa mamlaka yote katika nchi, na kupiga vita rushwa na ufisadi kwa nguvu zetu zote;

(4) Umoja ni nguvu ya pekee ya wananchi katika kujenga jamii yenye usawa na uhuru na katika kuondoa umaskini, ujinga, maradhi na kupambana na ufisadi.

(5) Uongozi bora unaozingatia ukweli, uzalendo, maadili ya uongozi na kuwajali wanyonge katika jamii ni sharti la msingi la kuendesha nchi

2.4.2 CCK ina malengo na madhumuni

(a) Kuhakikisha kwamba utajiri wa RASILIMALI tulizo nazo unatumika kwa maendeleo ya wananchi kwa kuondoa umasikini, ujinga na maradhi.

(b) Kuhakikisha kwamba uwekezaji unatekelezwa kwa kumnufaisha mwananchi kutokana na rasilimali alizo nazo na pia zinazomzunguka na kamwe usitoe mwanya na fursa kwa wageni kuhodhi rasilimali hizo bila ushiriki wa wananchi kwanza.

(c) Kuhakikisha kwamba shughuli za uchumi haziruhusu ulimbikizaji wa mali au njia kuu za uchumi kwa manufaa ya watu wachache binafsi.

(d) Kujenga umoja wa kitaifa kwa kutoa fursa sawa na za kutosha kwa wanajamiii wote bila kujali rangi, kabila dini au hali ya mtu.

(e) Kuhakikisha kwamba aina zote za dhuluma vitisho, ubaguzi, uonevu, rushwa, havipati tena nafasi baada ya kumwangamiza adui mkubwa UFISADI hapa nchini

(f) Kuhifadhi na kuendeleza mazingira kwa ajili ya uhai na afya ya binadamu na viumbe vingine na kwa faida ya vizazi vijavyo.

(g) Kulinda haki ya kila raia ya kujiendeleza kielimu au kutafuta elimu katika fani anayoipenda hadi kufikia mwisho wa upeo wa mtu.

(h) Kuhakikisha kuwa mfumo wetu wa uchaguzi ni huru na unatoa fursa stahikhi kwa wananchi kuchagua viongozi wanaowataka bila kurubuniwa kwa rushwa au takrima za aina yoyote ile.

(i) Kufufua maadili ya uongozi uadilifu na uwajibikaji kwa jamii ya Watanzania na kutenda haki katika Chama, kwa taswira ya weledi kama yalivyoainishwa na kusimamiwa na Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere katika uongozi wake Kitaifa.

(j) Kushinda katika chaguzi zote zitakazofanyika nchini kwa kutumia ushawishi wa nguvu ya hoja na kuunda serikali kuu na serikali za Mitaa hadi vitongoji katika pande zote mbili za Muungano ili kuiwezesha CCK Kutafsiri malengo na madhumuni yake kama yalivyoanishwa kwenye sura hii kwa vitendo

2.4.3 Itikadi za chama cha Kijamii.

(a) Uhafidhina wa kiuchumi na kijamii, mrengo wa kati kushoto,

(b) Lugha rasmi ya chama ni KISWAHILI na kitatiliwa mkazo mkubwa kwa matumizi ya hapa nchini na kwa Afrika nzima.

## 2.5 UANACHAMA NA UONGOZI NDANI YA CHAMA CHA KIJAMII

2.5.1 Sifa za mwanachama

(a) Awe ni raia wa Tanzania

(b) Ambaye ametimiza umri wa miaka 18

(c) Awe na akili timamu
(d) Ambaye anaiamini na kuikubali katiba pamoja na kutii kanuni zilizotungwa chini yake.
(e) Asiwe mwanachama wa Chama kingine cha siasa

2.5.2 Haki za mwanachama

(a) Kuchagua na kuchaguliwa ama kuteuliwa katika uongozi wa chama na ngazi yoyote.
(b) Kuhudhuria vikao au mikutano ya CCK ambayo mwanachama ni mjumbe
(c) Kupata habari zote zilizojadiliwa na kutolewa uamuzi na wanachama wenzie katika kumbukumbu za vikao vinavyomhusu.
(d) Kushiriki katika mijadala, shughuli na kazi za chama bila hofu wala upendeleo.
(e) Kutoa mapendekezo au taarifa ya kukiimarisha chama kwa njia ya mdomo au maandishi kwenye ofisi yoyote ya chama ngazi ya shina hadi Taifa kwa kuzingatia taratibu zilizowekwa.
(f) Kujitetea mbele ya kikao cha chama kinachohusika katika mashitaka au madai yoyote dhidi yake haki ambayo ni pamoja na fursa ya kukata rufani kwenye vikao vya juu iwapo hakuridhika na uamuzi wa kikao cha chini.
(g) Kumpigia kura mgombea wa CCK kwenye chaguzi ambazo CCK inashiriki za Kiserikali ngazi ya kijiji hadi Taifa.

2.5.3 Wajibu wa mwananchama

a) Kuielewa na kuitafsiri kwa matendo KATIBA ya CCK
b) Kuwa mkweli, mwaminifu, mwadilifu kwa kauli na vitendo
c) Kushiriki kikamilifu katika shunguli za Uongozi wa chama na kueneza sera na mipango (programu) za chama.
d) Kuwa tayari kujikosoa na kukosolewa ili kujiimarisha Kiitikadi au kiuongozi
e) Kulipa kiingilio na ada za kila mwezi kadri itakavyopitishwa na vikao husika vya CCK.
f) Kushiriki kikamilifu kwenye vikao vya Chama vinavyomruhusu.
g) Kujitoa muhanga kwenye shughuli za chama bila kutegemea malipo na kuwa tayari kukichangia Chama kwa hali na mali ili kuweza kujijenga na kukiimarisha
h) Kukuza moyo wa ushirikiano na kuheshimu maamuzi ya pamoja na kuyakubali
i) Kuwa mstari wa mbele katika kupambana na uvunjifu wa haki za binadamu na vitendo vyote vinavyoharibu maadili ya jamii yetu
j) Kujielimisha, kujiendeleza kielimu ili kuweza kukitumikia chama kwa ufanisi zaidi
k) Kukilinda chama kutokana na mitafaruku, majanga na vitendo vya kukigawa na kukidhoofisha chama.
l) Kuhakikisha kuwa ameandikishwa kama mpiga kura katika eneo analoishi

2.5.4 Ukomo wa Uanachama

Uanachama wa mtu unakoma mambo yafuatayo yakitokea.

a) Kujiuzulu kwa hiari yake mwenyewe
b) Kufukuzwa baada ya kukiuka nidhamu, maadili, wajibu unaotokana na Katiba ya Chama
c) Kwa kujiunga na chama kingine cha siasa
d) Kwa kushindwa kulipa ada na michango ya chama
e) Kwa kufariki dunia

2.5.5 Angalizo

Aliyejiuzulu au kufukuzwa uanachama atawajibika kurejesha mali au amana za chama alizo nazo na hatarejeshewa ofa au mchango wowote alioutoa kwenye chama. Aidha anaweza kuomba upya Uanachama kwa utaratibu ulioanishwa kwenye kanuni za chama

2.5.6 Sifa za kiongozi:

a) Awe na sifa zote za mwanachama kama zilivyoainishwa kwenye Katiba hii
b) Awe ana rekodi ya kutetea na kueneza katiba na sera za chama
c) Awe mchapakazi na mwenye uwezo wa kuongoza
d) Awe mkweli mwaminifu, mwadilifu na mnyenyekevu kwa viongozi wenzake na wanachama kwa kauli na vitendo pia awe mtetezi na mpenda haki asiye na historia ya ufisadi au uhalifu wa aina yoyote ile.
e) Awe na upeo mpana kiakili na kuwa tayari kujiendeleza yeye binafsi kielimu na kutumia elimu aliyoipata kuwaletea wananchi mabadiliko ya Kimaendeleo katika Jamii.
f) Awe na moyo na uwezo wa kufanyakazi na makundi mbalimbali ya jamii katika mazingira yoyote yale na kuwa mbunifu
g) Awe mtu aliye mstari wa mbele katika kujua matatizo ya jamii na kuyatafutia ufumbuzi.
h) Awe ni mzalendo na mwenye uchungu na nchi yake na awe na ushujaa na ushupavu wa kutetea masuala ya Msingi yanayogusa maslahi ya Taifa.
i) Asiwe mtu mwenye tamaa na rekodi ya ukigeugeu katika masuala ya kisiasa
j) Awe na rekodi ya nidhamu ya kuheshimu vikao, viongozi na wanachama kwa ujumla

2.5.7 Haki za kiongozi

a) Kujitetea katika kikao kinachoamua tuhuma dhidi yake kwa maandishi au kwa kuhudhuria yeye mwenyewe.
b) Kupinga hatua ya kufukuzwa kwake kwa kukata rufani kwenye kikao cha juu iwapo hakuridhika na uamuzi wa kikao cha chini
c) Kiongozi au mwanachama aliyefukuzwa au kurejeshwa na kikao kilichomfukuza au kikao cha juu baada ya kuridhishwa na mwenendo wa sababu zilizomfanya achukuliwe hatua kuwa amejirekebisha ama zimekoma.

2.5.8 Kuacha uongozi

Kiongozi atakoma kuwa kiongozi ikiwa mambo yafuatayo yatatokea

a) Muda wa Uongozi umemalizika
b) Amefukuzwa au kuachishwa kutokana na kukiuka Katiba ya chama, maadili, wajibu, nidhamu au sera za chama.
c) Kwa kujiuzulu mwenyewe au sababu zake binafsi
d) Amejiuzulu kutokana na Uamuzi wa wanachama walio wengi anaowaongoza kufuatia kupigiwa kura za kutokuwa na Imani naye kwa utendaji wake kwa mujibu wa Katiba / Kanuni za chama
e) Kupatikana na hatia mahakamani kwa kosa ambalo chama kitaona halistahiki kutendwa na kiongozi wa chama
f) Kwa kufariki

## SURA YA TATU

## VIKAO VYA CHAMA

### 3.1 VIKAO VYA CCK

3.1.1 Vikao vya shina

Shina litakuwa ni ngazi ya mwanzo kabisa katika muundo wa CCK, ngazi ambayo itakuwa ni eneo lolote lenye wanachama kuanzia (5) watano na hadi (30) thelathini

Ngazi ya Kitongoji

Katika maeneo ya vijijini kutakuwa na ngazi ya kitongoji ambayo itajumuisha eneo lote la Kitongoji lililo chini ya Mwenyekiti wa serikali ya Kitongoji.

3.1.2 Ngazi ya Tawi au Shehia

a) Katika maeneo ya Vijijini ya Tanzania Bara, Tawi litakuwa ni Eneo lote la Kijiji lililo chini ya Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji
b) Katika maeneo ya mijini ya Tanzania Bara, Tawi litakuwa ni eneo lote la Mtaa lililo chini ya Mwenyekiti wa serikali ya Mtaa.
c) Kwa Tanzania Zanzibar tawi litakuwa eneo la Shehia lililo chini ya Uongozi wa Serikali ya shehia.

3.1.3 Ngazi ya Kata au wadi

Kwa Tanzania Bara eneo lote la Kata lililo na Diwani kwa Zanzibar, Kata itakuwa sawa na Wadi.

3.1.4 Ngazi ya Wilaya yenye majimbo ya uchaguzi zaidi ya moja.

Wilaya itakuwa ni eneo lote lililochini ya mkuu wa wilaya wa Serikali. Endapo wilaya itakuwa na muundo wa Uongozi wa jimbo isipokuwa kwenye uwakilishi wa Kimkoa na Kitaifa litakuwa na uwakilishi wa Wilaya lenye majimbo mengi

3.1.5 Ngazi ya Mkoa.

Ngazi ya Mkoa itajumuisha eneo lote la Kimkoa lililochini ya Mkuu wa Serikali

3.1.6 Ngazi ya Taifa.

Ngazi ya Kitaifa itakuwa ni eneo lote la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

### 3.2. NGAZI YA SHINA

3.2.1 Shina litakua na wanachama wasiopungua watano (5) wanaoishi kwenye eneo moja au wanaofanya biashara kwenye eneo lenye vituo vya biashara.

3.2.2 Katika shina kutakua na Vikao vifuatavyo:-

a) Mkutano wa wanachama wote
b) Kamati ya uongozi
c) Kamati ya Nidhamu
d) Kamati ya Ulinzi na usalama

e) Vitengo vya chama
   i. Vijana
   ii. Wanawake
   iii. Wazee
   iv. Kitengo cha walemavi

3.2.3 Wajumbe wa mkutano wa wanachama wote
   a. Balozi wa Shina
   b. Katibu wa Shina
   c. Wanachama wote katika shina

3.2.4 Kazi za mkutano wa wanachama wote wa shina
   a. Kumchagua Mwenyekiti wa shina (Balozi) na Katibu wa shina unapofika wakati wa uchaguzi
   b. Kuchagua wajumbe wawili (2) wa kamati ya uongozi wa shina
   c. Kuchagua Mwenyekiti na makatibu wa vitengo kutoka miongoni mwa wanachama walio katika makundi hayo walioko kwenye shina siku ya uchaguzi
   d. Kuchagua wajumbe watatu (3) wa kila kamati za:-
      i. Ulinzi
      ii. Nidhamu
      iii. Usalama

   e. Kusimamia shughuli za chama na vitengo vya chama kuhakikisha kwamba vinafanya vikao kwa mujibu wa kanuni zao.
   f. Kupokea taarifa itakayowasilishwa kutoka kamati ya uongozi
   g. Kutekeleza maamuzi na maelekezo ya kikao cha juu
   h. Kueneza sera za CCK katika ngazi ya shina na nje ya shina pamoja na kushawishi raia waliofikia umri wa miaka kumi na minane (18) kujiunga na CCK
   i. Wakati wa uchaguzi wa kiserikali kuhakikisha kwamba wanachama wote katika Eneo lao wamejiandikisha kupiga kura na wanajitokeza kwenda kupiga kura kwa kuiwezesha CCK kupata ushindi.
   j. Shina litafanya vikao kama ifuatavyo:-
      i. Mkutano wa kawaida wa kiongozi uongozi kila mwezi
      ii. Mkutano wa mwaka
      iii. Mkutano maalumu wakati wowote kufuatana na hali ilivyo au kujitokeza.

3.2.5 Wajumbe wa kamati ya uongozi wa shina
   (a) Mwenyekiti (Balozi) wa shina
   (b) Katibu wa Shina
   (c) Wenyeviti wa kamati za Nidhamu, ulinzi na usalama
   (d) Wenyeviti na makatibu wa vitengo vya Vijana, wanawake na wazee katika shina
   (e) Wajumbe (2) wawili wa kamati ya Uongozi waliochaguliwa na mkutano wa wanachama wote katika shina.

3.2.6 Kazi za kamati ya uongozi
   a. Kuandaa orodha ya wanachama kila mara katika shina lao.
   b. Kuandaa orodha ya wapiga kura wote na kuithibitisha katika shina na kuwashawishi wajiandikishe na kuwajibika kumpigia kura mgombea wa CCK.
   c. Kubuni mbinu za kutatua kero za wanajamii bila kujali itikadi za kichama pia kutoa Elimu kwa wanachama wote kuhusu Katiba ya CCK

d. Kusimamia shughuli zote za kila siku za Chama kuanzia kwenye shina hilo kama zilivyoainishwa kwenye sura ya kwanza Ibara ya 2 ya Katiba hii.
e. Kuwasilisha taarifa ya maendeleo na shughuli za CCK ngazi ya shina na kutoa nafasi ya wanachama kuipokea na kuijadili
f. Kupokea taarifa za vitengo vya Chama na kamati ya Nidhamu ulinzi na usalama za shina na kuhakikisha kwamba vitengo vinafanya vikao kwa mujibu wa kanuni zao.
g. Kujadili na kufikia maamuzi kwa mwanachama ama kiongozi aliyekiuka maadili, wajibu pia kwenda kinyume na Katiba ya CCK na kusababisha kufukuzwa au kuachishwa, aidha kamati itaweza kumrudishia Uanachama au Uongozi kwa kuzingatia Katiba ya CCK sura ya pili Ibara ya 7:11 (c) (d) (e) 7.2 (f) wa shina
h. Kamati zote zitafanya vikao vyake kila mwezi

3.2.7 Kazi za Mwenyekiti wa shina (Balozi)
a. Ndiye msimamizi mkuu wa shughuli za Chama na msemaji mkuu katika shina
b. Ataongoza vikao vya mkutano wa wanachama wote na kamati ya uongozi wa shina.
c. Atakuwa na kura ya uamuzi, iwapo kura zitafungana

3.2.8 Kazi za katibu wa shina
a. Atakuwa ndiye mtendaji mkuu wa chama katika shina na kuwajibika kuchukua na kutunza kumbukumbu za vikao vyote vinavyomhusu.
b. Atatunza Daftari la orodha na kumbukumbu ya wanachama na wapiga kura
c. Atakuwa mdhibiti mkuu wa mali na miradi inayosimamiwa na Chama katika shina
d. Atakusanya ada na mapato mengine ya shina na kuyakabidhi kwa mweka hazina wa Tawi baada ya kutoa stakabadhi na kumkabidhi Mwanachama ama mfadhili.
e. Atafanya kazi zote kwa ushirikiano na mwenyekiti wa shina na atakazoelekezwa na mkutano wa wanachama wote na kamati ya uongozi wa shina
f. Atakuwa Katibu wa vikao vya mkutano wa wanachama wote na kamati ya uongozi katika shina.

## 3.3 NGAZI YA KITONGOJI

3.3.1 Katika Kitongoji kutakuwa na vikao vifuatavyo
a. Mtano mkuu wa wanachama wote
b. Kamati ya Uongozi wa kitongoji
c. Kamati ya ulinzi na usalama
d. Kamati ya Nidhamu
e. Vitengo vya Chama
   i. Vijana
   ii. Wanawake
   iii. Wazee

3.3.2 Wajumbe wa mkutano wa wanachama wote:-
(a) Mwenyekiti wa Kitongoji
(b) Katibu wa Kitongoji
(c) Wanachama wote wa CCK katika Kitongoji

3.3.3 Kazi za mkutano mkuu wa wanachama wote
a. Kumchagua mwenyekiti wa Kitongoji
b. Kumchagua Katibu wa Kitongoji
c. Kuchagua wajumbe watano (5) kwa kamati ya uongozi wa kitongoji.

d. Kuchagua wajumbe watano (5) wa kamati ya ulinzi na usalama.
e. Kuchagua wajumbe watatu (3) wa kamati ya Nidhamu
f. Kuchagu mjumbe mmoja (1) wa kuwakilisha kitongoji kwenye mkutano mkuu wa Kata wa CCK.
g. Kuchagua wajumbe wawili (2) watakaowakilisha kitongoji kwenye mkutano mkuu wa Tawi la CCK.
h. Kuteua wanachama madhubuti kuwa wasimamizi na mawakala wa mgombea/ wagombea katika vituo vya kujiandikisha kupiga kura na kuhakikisha kura za mgombea/wagombea wa CCK hazivurugwi wala haziibiwi na pia kufichua njama zote za udanganyifu.
i. Kuchagua wenyeviti makatibu wa vitengo vya Vijana, wanawake na wazee kutoka miongoni mwa wanachama walio katika makundi hayo wanaoishi katika kitongoji
j. Kuratibu shughuli za uongozi wa mashina katika eneo lao na kuwasilisha taarifa Tawini.
k. Kufanya kampeni kipindi cha uchaguzi wa Serikali ya Kitongoji kwa ushirikiano na viongozi wa Tawi na kuhakikisha mgombea / wagombea wa CCK ana/ wanaibuka na ushindi
l. Kitongoji kitafanya vikao vyake kama ifuatavyo:-

    i. Mkutano wa kawaida wa kamati ya uongozi kila mwezi
    ii. Mkutano Mkuu wa Mwaka
    iii. Mkutano maalum wakati wowote kufuatana na hali inayolazimu au kujitokeza (Dharura)

3.3.4 Wajumbe wa kamati ya Uongozi ya Kitongoji

(a). Mwenyekiti wa Kitongoji
(b). Katibu wa Kitongoji
(c). Mwenyekiti wa Serikali ya Kitongoji aliyechaguliwa kwa tiketi ya CCK.
(d) Wajumbe watano (5) waliochaguliwa na mkutano wa wanachama wote wa kitongoji
(e). Wenyeviti na makatibu wa vitengo vya chama
(f). Wenyeviti na makatibu wa kamati ya Nidhamu, ulinzi na usalama.
(g) Mjumbe anayewakilisha kitongoji kwenye mkutano mkuu wa Kata

3.3.5 Kazi za kamati ya Uongozi

(a) Kuwaandaa na kuwashawishi wanachama wenye uwezo na kukubalika na wanajamii ili waweze kugombea nafasi za uongozi wa serikali kwa tiketi ya CCK
(b) Kujadili maendeleo ya chama na miradi inayoendeshwa na chama pamoja na vitengo vya CCK
(c) Kuwa na orodha ya wanachama wote wanoishi katika kitongoji wenye haki ya kupiga kura na kuhakikisha kwamba wakati wa uchaguzi wanajitokeza kupiga kura bila kukosa.
(d) Kumfukuza na kumsimamisha mwanachama au kiongozi kwa kukiuka maadili na Katiba ya CCK, aidha kujadili na kusikiliza rufani zitakazoletwa na mwanachama au kiongozi na kuzipatia ufumbuzi kwa mujibu wa Katiba.
(e) Kupokea na kuzifanyia kazi taarifa za Vitengo kama zitakavyowasilishwa na kuhakikisha pia vinafanya vikao kwa mujibu wa kanuni zao.
(f) Kamati ya uongozi wa kitongoji itafanya vikao vyake kila mwezi

(g) Kusimamia ustawi wa mashina

## 3.4 NGAZI YA TAWI

3.4.1 Tawi litakuwa na vikao vifuatavyo:-

(a) Mkutano mkuu wa Tawi
(b) Kamati ya uongozi ya tawi
(c) Kamati ya ulinzi na usalama
(d) Kamati ya Nidhamu
(e) Vitengo vya chama
   i. Vijana
   ii. Wanawake
   iii. Wazee
   iv. Walemavu

3.4.2 WAJUMBE WA MKUTANO MKUU WA TAWI

a) Mwenyekiti
b) Katibu
c) Mweka Hazina
d) Mwenyekiti serikali za Mitaa /Kijiji na Vitongoji waliochaguliwa kwa tiketi ya CCK
e) Wajumbe wa serikali za mitaa Kijiji na Vitongoji waliochaguliwa kwa tiketi ya CCK
f) Wajumbe wawili (2) wanaowakilisha kitongoji
g) Wenyeviti wa kamati ya Nidhamu na Ulinzi na usalama
h) Wenyeviti na makatibu wa vitengo vya Chama
i) Wanachama wote kutoka mashina yaliyopo katika tawi hilo

3.4.3 KAZI ZA MKUTANO WA TAWI

(a) Kupokea taarifa ya kamati ya uongozi ya tawi na kujadili taarifa ya miezi mitatu ya kazi za chama tawini
(b) Kumchagua Mwenyekiti wa tawi unapofikia wakati wa uchaguzi
(c) Kupitisha mipango mbalimbali ya chama itakayoelekeza kunufaisha maslahi ya wanajamii
(d) Kupokea na kujadili taarifa ya fedha za chama katika tawi
(e) Kupokea taarifa za kamati ya Nidhamu, Ulinzi na usalama na vitengo vya chama katika tawi
(f) Kuchagua wajumbe watano (5) wa kamati ya Uongozi ya Tawi.
(g) Kuchagua wajumbe watatu (3) wa kuwakilisha kwenye mkutano mkuu wa Kata
(h) Kuchagua wajumbe wanne (4) wa kamati za Nidhamu, ulinzi na usalama kwa kila kamati.
(j) Kuchagua miongoni mwa wnachama waaminifu na wanaofaa kuwa wasimamizi / mawakala wa wagombea wa CCK wakati wa chaguzi za Kiserikali.
(k) Kuratibu na kusimamia kwa karibu shughuli za vitengo vya chama katika tawi.
(l) Kumchukulia hatua za kinidhamu mwanachama au kiongozi yoyote ndani ya Tawi kwa kumsimamisha au kumuachisha/ kumfukuza uongozi mwanachama iwapo atakiuka katika, maadili na nidhamu ya chama.
(m) Mkutano mkuu wa Tawi ndio utakaokuwa na maamuzi ya mwisho katika mambo yote ya chama yanayohusiana na Tawi husika.
(n) Kuhakikisha kwamba Tawi linakuwa na ofisi ya CCK na inafanya kazi kikamilifu
(o) Tawi litafanya vikao vyake kama ifuatavyo:-
   I. Mkutano wa kawaida wa kila baada ya miezi miwili
   II. Mkutano mkuu wa mwaka.

III. Mkutano maalumu wakati wowote kufuatana na hali inavyolazimika au kujitokeza (dharura)

3.4.4 Wajumbe wa kamati ya uongozi ya Tawi:-

a) Mwenyekiti wa Tawi
b) Katibu wa Tawi
c) Mwekahazina wa Tawi
d) Wenyeviti na makatibu wa vitongoji vilivyopo katika Tawi.
e) Wenyeviti na makatibu ya kamati ya nidhamu, ulinzi na usalama katika Tawi.
f) Wenyeviti na makatibu wa vitengo vya CCK vya Tawi waliochaguliwa kwa mujibu wa kanuni za vitengo vyao.
g) Wenyeviti wa Serikali za Vitongoji waliochaguliwa kwa tiketi ya CCK
h) Wenyeviti wa Serikali ya Kijiji / Mtaa aliyechaguliwa kwa tiketi ya CCK
i) Diwani anayeishi eneo la Tawi aliyechaguliwa kwa tiketi ya CCK
j) Mbunge au mwakilishi wa CCK anayeishi eneo la Tawi husika.
k) Wajumbe watano (5) waliochaguliwa na mkutano mkuu wa Tawi
l) Wajumbe watatu (3) Waliochaguliwa na mkutano mkuu wa Tawi kuwakilisha Tawi kwenye mkutano mkuu wa kata.
m) Wenyeviti na makatibu wa mashina ya CCK
n) Mjumbe au Wajumbe wa kamati kuu ya Taifa waliopo kwenye eneo la Tawi hilo.

3.4.5 Kazi za kamati ya uongozi wa Tawi:-

a) Kuwachagua katibu na mweka hazina wa Tawi.
b) Kusimamia utekelezaji wa sera na kutetea itikadi ya chama kabla na baada ya wakati wa kampeni za uchaguzi wa Kiserikali
c) Kusimamia mapato na matumizi ya fedha katika Tawi
d) Kubuni na kusimamia vyanzo vya mapato ya Tawi na miradi ya chama iliyoidhinisha na kamati ya uongozi ya Tawi.
e) Kuchambua matatizo ya wanajamii kisiasa na kiuchumi yaliyopo katika eneo la Tawi hilo na kuchukua hatua za kuelimisha na kupendekeza kisha kutatua kero kwa kushirikiana na wananchi husika.
f) Kutetea kwa nguvu zote haki za binadamu na haki za makundi kama wanawake, watoto, wazee na walemavu.
g) Kutambua namna bora ya kuwashirikisha wanawake, vijana wa CCK katika uzalishaji mali kwa manufaa yao na chama kwa pamoja.
h) Kuongoza katika eneo lake, harakati za kupinga uonevu unaoweza kufanywa na Serikali au kikundi chochote na kuwaelekeza wananchi jinsi ya kupata, kutetea na kulinda haki zao.
i) Kuwaandaa wanachama kushirikiana na wananchi wengine katika kuleta Demokrasia ya kweli na yenye maendeleo kwa kushirikiana na vyama vya wanajamii hapo walipo.
j) Kupitia majina ya wanaoomba kugombea uongozi wa Serikali za vitongoji na kuyawasilisha kwenye mkutano Mkuu wa mwaka wa Tawi.
k) Kumjadili kiongozi au mwanachama aliyejiudhuru na ambaye ameomba kurudi katika chama ama uongozi.
l) Kusimamia mapato na matumizi ya fedha za chama katika Tawi.
m) Kusimamia kwa ukaribu uundwaji na uchaguzi wa viongozi wa mashina na vitongoji kwa mujibu wa katiba ya CCK.
n) Kusikiliza malalamiko juu ya uongozi wa mashina na vitongoji na kuchukua hatua za kinidhamu pale itakapobidi, aidha aliyechukuliwa hatua aweza kukata rufaa kwenye ngazi ya mkutano mkuu wa Tawi ndani ya siku kumi na nne (14)

o) Kamati ya uongozi wa Tawi itafanya vikao vyake kila baada ya miezi miwili (2) au wakati wowote kwa dharura.

## 3.5 NGAZI YA KATA

3.5.1 Kata itakuwa na vikao vifuatavyo:-

a) Mkutano mkuu
b) Kamati kuu
c) Kamati ya utendaji
d) Kamati ya nidhamu
e) Kamati ya ulinzi na usalama.
f) Vitengo vya chama:-
    (i) Vijana
    (ii) Wanawake
    (iii) Wazee
    (iv) Walemavu

3.5.2 Wajumbe wa mkutano Mkuu wa Kata:-

a) Mwenyekiti wa kata
b) Katibu wa kata
c) Mhazini
d) Katibu Mwenezi
e) Katibu Mipango
f) Wenyeviti na makatibu wa matawi
g) Wenyeviti na makatibu wa Vitongoji ngazi ya Kata
h) Wenyeviti na makatibu wa vitengo vya chama ngazi ya tawi na Kata.
i) Mjumbe aliyechaguliwa na mkutano mkuu wa Kitongoji
j) Wajumbe wawili (2) waliochaguliwa na mkutano mkuu wa Tawi.
k) Diwani aliyechaguliwa kwa tiketi ya CCK
l) Wenyeviti wa Serikali za vijiji, mitaa na vitongoji waliochaguliwa kwa tiketi ya CCK.
m) Wenyeviti na makatibu wa vitengo vya chama katika ngazi ya kata.
n) Wajumbe watano (5) waliochaguliwa na mkutano mkuu wa kila Tawi
o) Wajumbe watano (5) wanaowakilisha kata kwenye mkutano mkuu wa Wilaya
p) Wajumbe kumi (10) wa kamati kuu waliochaguliwa na mkutano mkuu wa kata.
q) Wajumbe watano (3) wanaowakilisha Kata kwenye mkutano mkuu wa Mkoa.

3.5.3 Kazi ya Mkutano mkuu wa Kata:-

a) Kutoa taarifa, miongozo na mikakati inayohusu maendeleo ya chama katika Kata.
b) Kupima na kuratibu utekelezaji wa shughuli za chama kwenye matawi ya CCK.
c) Kutangaza majina ya wagombea wa nafasi ya uenyekiti wa Serikali za vitongoji, Vijiji na Mitaa.
d) Kuchagua wajumbe watano (5) wanaowakilisha Kata kwenye Mkutano mkuu wa Wilaya.
e) Kuchagua wajumbe kumi (10) wa kamati kuu ya Kata.
f) Kumchagua mwenyekiti na Mhazini wa Kata.
g) Kumchagua Katibu Mwenezi na Katibu Mipango wa Kata
h) Kuhakikisha kuwa wakati wa uchaguzi mawakala wanaofaa wanapatikana ili kuweza kulinda kura za wagombea wa CCK.

i) Kuhakikisha kuwa Kata inakuwa na ofisi ya CCK, na inafanyakazi kikamilifu kila siku.
j) Kata inafanya vikao vyake kama ifuatavyo:-
   i. Mkutano wa kila baada ya miezi mitatu (3)
   ii. Mkutano mkuu wa mwaka
   iii. Mkutano maalumu wakati wowote kufuatana na hali inavyolazimu au kujitokeza (dharura)

3.5.4 Wajumbe wa kamati kuu ya kata:-

a) Mwenyekiti wa Kata.
b) Katibu wa Kata.
c) Mhazini wa Kata.
d) Wajumbe kumi (10) waliochaguliwa na mkutano mkuu wa Kata.
e) Wajumbe watano (5) wanaowakilisha Kata katika Mkutano mkuu wa Wilaya.
f) Wenyeviti na makatibu wa vitengo vya CCK ngazi ya Kata.
g) Diwani aliyechaguliwa kwa tiketi ya CCK
h) Wenyeviti wa Serikali za vitongoji, vijiji na mitaa waliochaguliwa kwa tiketi ya CCK.
i) Wenyeviti na makatibu wa matawi ya CCK yaliyomo katika Kata.
j) Katibu uenezi na katibu mipango wa Kata
k) Mbunge aliyechaguliwa kwa tiketi ya CCK anayeishi kwenye Kata hiyo.
l) Mjumbe wa kamati kuu ya Taifa au kiongozi wa ngazi ya kitaifa Wanaoishi kwenye Kata hiyo.
m) Wajumbe wa watano kamati ya utendaji ya Kata

3.5.5 Kazi za kamati kuu ya Kata:-

a) Kusimamia mapato na matumizi ya fedha za chama katika Kata.
b) Kuchagua wajumbe watano (5) wa kamati ya utendaji wa Kata.
c) Kuhamasisha wananchi kwenda kupiga kura na wanachama kugombea uongozi ndani ya CCK.
d) Kusimamia kwa karibu utekelezaji wa Sera za chama katika Kata.
e) Kupokea, kujadili na kutoa maamuzi juu ya utendaji wa shughuli za chama kwenye matawi yaliyomo kwenye Kata.
f) Kupiga kampeni kwa uwezo na nguvu zote ili kuhakikisha kwamba wagombea wa CCK wanashinda katika chaguzi za Kiserikali.
g) Kutathimini na kutoa mapendekezo yanayohusu hali ya kisiasa, kiuchumi na kijamii na kuyawasilisha ngazi ya Wilaya.
h) Kuhakikisha kwamba matawi ya CCK yanakusanya ada na michango mbalimbali kutoka kwa wanachama kama ilivyoamliwa na CCK.
i) Kuhakikisha kwamba kamati ya nidhamu, ulinzi na usalama pamoja na vitengo vya CCK ngazi ya Kata wanafanya vikao vyao kwa mujibu wa kanuni na taratibu zao na kutoa taarifa zao kwenye chama ngazi ya Kata.
j) Kamati ya kuu ya Kata itafanya vikao vyake mara moja kila baada ya miezi mitatu (3)

3.5.6 Wajumbe wa kamati ya utendaji ya Kata:-

a) Mwenyekiti wa Kata
b) Katibu wa Kata

c) Mhazini wa Kata
d) Katibu uenezi na Katibu Mipango
e) Wajumbe watano (5) waliochaguliwa na kamati kuu ya Kata
f) Wenyeviti na makatibu wa vitengo vya CCK
g) Wenyeviti wa kamati ya Nidhamu, Ulinzi na Usalama wa ngazi ya Kata.
h) Diwani aliyechaguliwa kwa tiketi ya CCK
i) Mbunge anayeishi katika Kata hiyo.

3.5.7 Kazi za kamati ya utendaji ya Kata:-

a) Kusimamia shughuli za kila siku za utekelezaji katika chama ndani ya Kata.
b) Kubuni mikakati ya kuhamasisha wananchi kwa shabaha ya kutafuta kuungwa mkono na kushawishi wananchi ili waweze kugombea nafasi mbalimbali za Kiserikali kwa tiketi ya CCK.
c) Kufuatilia matatizo ya kijamii katika Kata kwa madhumuni ya kuandaa sera ya CCK.
d) Kufuatilia ahadi zilizotolewa na wagombea uongozi wa Serikali kwa tiketi ya CCK na kuishauri kamati kuu ya Kata.
e) Kutathimini maendeleo ya shughuli za CCK katika Kata na kuishauri kamati kuu ya Kata hatua za kufanya.
f) Kuamua juu ya matatizo na rufaa kutoka ngazi za chini.
g) Kujadili na kutoa mapendekezo ya wanaogombea udiwani na kuyawasilisha kwenye kamati kuu ya Kata.
h) Kamati ya utendaji ya Kata itakutana mara moja kila baada ya miezi miwili (2) katika vikao vyake vya kawaida, na inawezekana kufanya kikao chake wakati wowote inapobidi.

## 3.6 NGAZI YA WILAYA YENYE MAJIMBO YA UCHAGUZI ZAIDI YA MOJA.

3.6.1 Wilaya itakuwa na vikao vifuatavyo:-

a) Mkutano mkuu wa Wilaya.
b) Kamati kuu ya Wilaya
c) Kamati ya utendaji ya Wilaya.
d) Kamati ya nidhamu, ulinzi na usalama.
e) Vitengo vya chama:-
    i. Vijana
    ii. Wanawake
    iii. Wazee
    iv. Walemavu

3.5.8 Wajumbe wa mkutano mkuu wa Wilaya:-

a) Mwenyekiti wa Wilaya
b) Katibu wa Wilaya
c) Mhazini wa Wilaya
d) Katibu uenezi wa Wilaya
e) Katibu Mipango na Uchumi wa Wilaya
f) Wenyeviti na Makatibu wa Kata
g) Makatibu uenezi wa Kata
h) Makatibu mipango na uchumi wa Kata
i) Wenyeviti na makatibu wa kamati ya nidhamu na ulinzi na usalama wa

Wilaya.

j) Wajumbe wa kamati ya utendaji ya Wilaya (5)
k) Wawakilishi, Wabunge na Madiwani kwa tiketi ya CCK
l) Wajumbe watano (5) wa kuchaguliwa kutoka kila Kata.
m) Wajumbe watatu (3) wanaowakilisha Wilaya kwenye mkutano mkuu wa Taifa
n) Wajumbe wanne (4) wanaowakilisha Wilaya kwenye mkutano mkuu wa Mkoa.
o) Mjumbe wa kamati kuu ya Taifa anayeishi katika Wilaya hiyo
p) Wenyeviti wa Halmashauri za manispaa na miji kwa tiketi ya CCK.

3.5.9 Kazi za mkutano Mkuu wa Wilaya:-

a) Kupokea taarifa ya kazi za chama kutoka kwenye Kata.
b) Kutoa miongozo na mikakati inayohusu maendeleo ya CCK katika Kata na kuhakikisha kwamba utekelezaji wake unakamilishwa.
c) Kumchagua mwenyekiti wa Wilaya
d) Kuwachagua Mhazini, Katibu Uenezi, Katibu Mipango na Uchumi wa Wilaya.
e) Kuchagua wajumbe kumi (10) wa kamati ya utendaji wa Wilaya.
f) Kuchagua wajumbe kumi (10) wa kamati kuu ya CCK Wilaya.
g) Kuchagua wajumbe wanne (4) wanaowakilisha Wilaya kwenye mkutano mkuu wa Mkoa
i. Kuchagua wajumbe watatu (3) wanaowakilisha Wilaya kwenye mkutano mkuu wa Taifa
h) Kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya kiongozi wa kata au wa ngazi ya chini iwapo atabainika kwamba anakiuka Katiba, maadili na nidhamu ya CCK.
i) Kusikiliza rufaa kutoka kwa viongozi na wanachama wa CCK waliochukuliwa hatua za kinidhamu
j) Kuhakikisha chama kina ofisi ya kudumu na inafanyakazi ipasavyo kila siku.
k) Wilaya itafanya vikao vyake kama ifuatavyo:-
    i. Mkutano wa kila baada ya miezi mitatu.
    ii. Mkutano mkuu wa mwaka
    iii. Mkutano maalumu wakati wowote kufuatana na hali inavyolazimu au kujitokeza (dharura)

3.5.10 Wajumbe wa kamati kuu ya Wilaya:-

a) Mwenyekiti wa Wilaya
b) Katibu wa Wilaya
c) Mhazini wa Wilaya
d) Katibu Uenezi wa Wilaya
e) Katibu Mipango na Uchumi wa Wilaya
f) Wajumbe kumi (10) waliochaguliwa na mkutano mkuu wa Wilaya
g) Wajumbe watatu (3) wanaowakilisha Wilaya kwenye mkutano mkuu wa Taifa.
h) Wajumbe wanne (4) wanaowakilisha Wilaya kwenye mkutano mkuu wa Mkoa
i) Mwenyekiti na katibu wa kamati ya Nidhamu ya Wilaya
j) Mwenyekiti na Katibu wa kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya
k) Wenyeviti na Makatibu wa Vitengo vya chama wa Wilaya
l) Wenyeviti na Makatibu wa CCK ngazi ya kata
m) Wabunge, Madiwani na Wawakilishi na pia Wenyeviti wa Halmashauri za wilaya Miji na Manispaa kwa tiketi ya CCK katika Wilaya.

3.6.5 Kazi za kamati kuu ya Wilaya

(a) Kusimamia mapato na matumizi ya fedha za chama katika Wilaya na kuwasilisha taarifa hiyo kwenye mkutano mkuu wa Wilaya
(b) Kutekeleza sera za CCK katika Wilaya
(c) Kuchagua mweka hazina wa Wilaya, katibu uenezi na katibu mipango na uchumi wa Wilaya
(d) Kusimamia vema kampeni za uchaguzi ili CCK kiweze kupata ushindi kwenye chaguzi za Kiserikali.
(e) Kupokea miongozo ya Chama toka ngazi za juu na kuwasilisha utekelezaji wake ngazi za chini za CCK.
(f) Kupitia majina ya wagombea ubunge na udiwani na kuyapeleka ngazi ya Taifa ya CCK.
(g) Kumsimamisha kiongozi wa CCK ngazi ya Tawi na kata ambaye atabainika kwamba anakiuka maadili na nidhamu ya chama.
(h) Kuhakikisha kwamba CCK inakua na ofisi ya kudumu ya Wilaya na inafanyakazi kikamilifu
(i) Kamati kuu ya Wilaya itafanya vikao vyake mara moja kila baada ya miezi mitatu

3.5.11 Wajumbe wa Kamati ya utendaji ya Wilaya

a) Mwenyekiti wa Wilaya
b) Katibu wa Wilaya
c) Mweka hazina wa Wilaya
d) Katibu uenezi wa Wilaya
e) Katibu mipango na uchumi wa wilaya

3.6.7 Kazi za Kamati ya utendaji

a) Kutekeleza shughuli za kila siku za chama Wilayani
b) Kupokea taarifa za utendaji za kata
c) Kuweka mikakati ya Kampeni za uchaguzi katika Wilaya
d) Kuratibu shughuli za Chama kwenye Kata
e) Kuamua juu ya rufaa zinazotoka ngazi za chini za CCK
f) Kuteua na kutangaza majina ya wagombea udiwani baada ya kupata maoni ya kamati kuu ya chama ya Kata
g) Kupitia na kutoa maoni juu ya wagombea ubunge katika majimbo ya Wilaya hiyo.
h) Kuwasiliana na Kata juu ya taarifa muhimu za uchaguzi wa Kiserikali
i) Kusimamia na kuandaa mapato na matumizi ya CCK. Katika Wilaya na kuwasilisha taarifa yake kwenye kamati kuu ya Wilaya kwa kujadiliwa.
(j) Kamati ya utendaji itafanya vikao vyake mara moja kila baada ya miezi 2 au wakati wowote ikiwa ni lazima (Dharura).

## 3.7 NGAZI YA MKOA

3.7.1 Mkoa utakuwa na vikao vifuatavyo

a) Mkutano mkuu wa Mkoa
b) Kamati kuu ya Mkoa
c) Kamati ya utendaji ya Mkoa
d) Kamati ya ulinzi na usalama

e) Vitengo vya Chama
   i. wanawake
   ii. Vijana
   iii. Wazee
   iv. Walemavu

3.7.2 Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Mkoa

(a) Mwenyekiti wa Mkoa
(b) Katibu wa Mkoa
(c) Mhazini wa Mkoa
(d) Katibu uenezi wa Mkoa
(e) Katibu mipango na uchumi wa Mkoa
(f) Wenyeviti na makatibu wa Kamati ya Nidhamu ulinzi na usalama za Mkoa na Wilaya na Kata
(g) Wenyeviti na makatibu waweka hazina na makatibu mipango na makatibu Uenezi wa Wilaya
(h) Wenyeviti makatibu waweka hazina na Makatibu mipango na makatibu uenezi wa wilaya
(i) Wajumbe wa kamati kuu ya Mkoa kumi (10)
(j) Wajumbe watatu (3) wanaotoka wilayani kwenda kwenye mkutano mkuu wa Taifa.
(k) Wajumbe watatu (3) kutoka kila Kata na Wilaya wanaowakilisha kwenye mkutano mkuu wa Mkoa
(l) Meya au Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya aliyechaguliwa kwa tiketi ya CCK

3.7.3 Kazi za Mkutano Mkuu wa Mkoa

a) Kutoa Miongozo na mikakati inayohusu maendeleo ya Chama katika Mkoa.
b) Kumchagua Mwenyekiti wa Mkoa
c) Kuwachagua wajumbe (10) kumi wa kamati kuu ya Mkoa
d) Kuwachagua wajumbe watatu (3) wa mkutano mkuu wa Taifa
e) Kupokea taarifa za maendeleo ya kazi za Chama kutoka ngazi za kata na wilaya na kutoa maelekezo ya utekelezaji.
f) Kuhakikisha kwamba mkoa unakua na ofisi ya kudumu na kufanya kazi ipasavyo
g) Mkoa utakuwa na vikao vyake mara moja kila baada ya miaka miwili na nusu. Lakini unaweza kukutana wakati wowote ikibidi (Dharura)

3.7.4 Wajumbe wa kamati kuu ya Mkoa

a) Mwenyekiti wa Mkoa
b) Katibu wa Mkoa
c) Mhazini wa Mkoa
d) Katibu Uenezi na Katibu Mipango na Uchumi wa Mkoa.
e) Wenyeviti na Makatibu wa kamati ya Nidhamnu, Ulinzi na Usalama wa Wilaya na Mkoa.
f) Wenyeviti na Makatibu wa Vitengo vya Chama Mkoa na Wilaya
g) Wajumbe watatu (3) wanaowakilisha Mkoa kwenye mkutano mkuu wa Taifa
h) Wabunge au wawakilishi kwa tiketi ya CCK
i) Wenyeviti na makatibu wa Wilaya CCK

3.7.5 Kazi za Kamati kuu ya Mkoa

a) Kusimamia utekelezaji wa maamuzi yaliyotolewa na kamati kuu ya Taifa na mkutano Mkuu wa Mkoa
b) Kuweka mikakati ya utekelezaji wa sera za CCK katika Mkoa
c) Kuchagua Mhazini, Katibu Uenezi na Katibu Mipango na Uchumi wa Mkoa
d) Kupokea mapendekezo ya makisio ya mapato na matumizi ya CCK toka kwenye kamati ya utendaji ya Mkoa
e) Kupanga matumizi ya chama ya Mkoa na kuyasimamia ipasavyo
f) Kusimamia kamati kuu za Wilaya na kufuatilia utendaji wa kazi hizo
g) Kuhakikisha kwamba Mkoa unakuwa na ofisi kuu ya kudumu ya CCK na inafanya kazi ipasavyo.
h) Kamati kuu ya Mkoa itakutana mara moja kila baada ya miezi minne ndani ya mwaka. Lakini inaweza kufanya kikao wakati wowote ikibidi (Dharura )

3.7.6 Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya Mkoa

a) Mwenyekiti wa Mkoa
b) Katibu wa Mkoa
c) Mhazini wa Mkoa
d) Katibu Uenezi na Katibu Mipango na Uchumi wa Mkoa
e) Wakuu wa Taasisi za CCK
f) Wajumbe watano (5) waliochaguliwa na Kamati Kuu ya Mkoa.
g) Wenyeviti na Makatibu wa Vitengo vya Chama Mkoa
h) Wenyeviti na Makatibu wa Kamati za Nidhamu na Ulinzi na Usalama za Mkoa

3.7.7 Kazi za Kamati ya Utendaji ya Mkoa

a) Kutekeleza shughuli za kila siku za CCK chini ya uongozi wa Mkoa
b) Kupokea taarifa za utendaji za Wilaya na kuzifikisha kwenye kamati kuu ya Mkoa kwa hatua zaidi
c) Kusimamia shughuli za uenezi, uhamasishaji na kampeni
d) Kuchuja majina ya wagombea uongozi ya Kata na Wilaya kwa nia ya kupata wagombea wenye sifa.
e) Kusikiliza rufaa mbalimbali na kuzitolea maamuzi kutoka ngazi za Kata na Wilaya.
f) Kumchukulia hatua za kinidhamu kiongozi yeyote wa ngazi ya Mkoa, Wilaya na Kata iwapo itadhihirika kwamba anakiuka Katiba, Madili na Nidhamu ya CCK
g) Aliyechukuliwa hatua anaweza kukata rufani ndani ya kipindi cha siku 14 baada ya kupewa taarifa ya hatua hiyo.
h) Kamati ya utendaji itakutana kila baada ya miezi miwili (2) au kwa Dharura.

## 3.8 NGAZI YA TAIFA

3.8.1 Kutakuwa na Vikao vya Taifa Vifuatavyo:-

a) Mkutano mkuu wa Taifa
b) Kamati kuu ya Taifa
c) Sekretarieti.
d) Kamati ya Utendaji ya Taifa
e) Vitengo vya Chama
    i. Wanawake
    i. Vijana

ii. Wazee
iii. Walemavu

f) Kamati ya Nidhamu
g) Kamati ya Ulinzi na Usalama

3.8.2 Wajumbe wa Mkutano mkuu wa Taifa.

a) Mwenyekiti wa Taifa
b) Makamu mwenyekiti Tanzania Bara
c) Makamu Mwenyekiti Tanzania Zanzibar
d) Katibu Mkuu wa Taifa
e) Katibu Kiongozi ofisi ya katibu Mkuu na Naibu Katibu Kiongozi ofisi ya Naibu Katibu Mkuu Tanzania Zanzibar.
f) Mweka Hazina na Manaibu wawili mmoja wa Bara na mwingine wa Zanzibar
g) Katibu Mipango wa Uchumi na manaibu wawili mmoja wa Bara na Mwingine Zanzibar
h) Katibu Mwenezi na manaibu wawili mmoja wa Bara na Mwingine Zanzibar
i) Wenyeviti na makatibu wa mikoa na makatibu wa wilaya
j) Wenyeviti na makatibu wa vitengo vya Chama ngazi ya Mkoa na Taifa
k) Wajumbe kumi (10) kumi walioteuliwa na Mwenyekiti wa Taifa.
l) Wajumbe watatu (3) waliochaguliwa toka kila Wilaya
m) Wajumbe watatu (3) waliochaguliwa na Mkoa
n) Wabunge na wawakilishi wote walioingia bungeni kwa tiketi ya CCK.
o) Wajumbe wa Bodi ya wadhamini ya CCK

3.8.3 Kazi za mkutano mkuu wa Taifa

a) Kumchagua Mwenyekiti wa CCK Taifa
b) Kuwachagua Makamu Wenyeviti wa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar
c) Kuteuliwa na kupitishwa kwa katibu mkuu wa CCK Taifa.
d) Kupokea na kujadili taarifa zote zilizowasilishwa na kamati kuu ya CCK Taifa na kutoa maelekezo ya utekelezaji wake katika ngazi zote za CCK.
e) Kupitisha sera za Chama na Mipango yake (programu) na kuagiza utekelezaji.
f) Mkutano mkuu wa CCK utakuwa na uwezo wa kutunga katiba au kubadili sehemu yoyete ya Katiba ya Chama kwa uamuzi wa theluthi mbili (2/3) ya wajumbe wenye haki ya kupiga kura.
g) Kuidhinisha ama kuchagua wajumbe kumi (10) wanaoteuliwa na Mwenyekiti wa Taifa kwa uwiano wa wajumbe watano (5) kutoka Bara na kati yao Wanawake ni wawili (2) na watano (5) kutoka Zanzibar kati yao wanawake watatu (3), kuwa wajumbe wa mkutano mkuu wa taifa.
h) Wajumbe wa Mkutano Mkuu wanaotoka Zanzibar watapendekeza majina mawili kwenye mkutano mkuu ambayo yatapigiwa kura kwa lengo la kumpata makamu mwenyekiti wa Taifa Zanzibar.
i) Mkutano mkuu wa Taifa unaweza kukasimu kazi na madaraka yake kwa kikao au chombo chochote cha CCK yaani Kamati Kuu au Kamati ya utendaji
j) Kufanya tathimini na kutoa mikakati juu ya mipango ya kukiimarisha chama Nchini kote
k) Kujadili na kuridhia itikadi falsafa na Sera za CCK na kuweka mikakati na miongozo ya kiutekelezaji.
l) Kuthibitisha au kutengua uamuzi wowote uliofanywa na kikao cha CCK ngazi ya chini
m) Kupokea rufaa na kuzitolea maamuzi sahihi rufaa hizo

n) Kumvua uanachama au uongozi kiongozi yeyote ikiwa ni pamaoja na Mwenyekiti Taifa endapo itadhihirika kwamba anakiuka Katiba, maadili na nidhamu ya CCK.
o) Maamuzi yatakayofanywa na mkutano mkuu yatakuwa halali iwapo zaidi ya nusu ya wajumbe waliohudhuria na wenye uhalali wa kupiga kura wataunga mkono
p) Mkutano mkuu wa Taifa utafanyika mara moja kila baada ya miaka mitano (5) lakini unaweza kuitishwa na kufanyika usio wa kawaida kwa kuitishwa na Mwenyekiti wa Chama Taifa kwa mashauriano ya pamoja na kamati Kuu ya Taifa.

3.8.4 Wajumbe wa Kamati Kuu ya Taifa

a) Mwenyekiti wa Taifa
b) Makamu Mwenyekiti Bara na Zanzibar
i) Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu Zanzibar pamoja na Katibu Kiongozi ofisi ya Katibu Mkuu/Bara na Zanzibar
c) Mweka Hazina na Manaibu weka
d) Katibu Uenezi na manaibu Katibu Uenezi
e) Katibu Mipango na manaibu Katibu mipango
f) Wakuu wa Idara za chama
g) Wenyeviti na makatibu wa vitengo vya CCK ngazi ya Taifa
h) Wajumbe wa Baraza la Wadhamini la CCK
i) Wenyeviti na Makatibu wa Wabunge wa Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wawakilishi wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar na Bunge la Afrika kwa tiketi ya CCK
j) Wajumbe watano (5) watakaoteuliwa na Mwenyekiti Taifa.

3.8.5 Kazi za Kamati Kuu ya Taifa

a) Kutunga sera za maendeleo na utatuzi wa kero za jamii na kiuchumi zitakazogusa kila sekta na makundi yote na kuziwasilisha kwenye mkutano mkuu wa Taifa
b) Kutekeleza sera za CCK kama zilivyokubaliwa na kupitishwa na mkutano mkuu wa Taifa.
c) Kufanya ufuatiliaji wa kutosha wa kitaifa na kuhakikisha kwamba sera za CCK zinatekelezwa kikamilifu na kuzaa matunda yaliyokusudiwa.
d) Kutathimini utekelezaji wa shughuli zote za CCK Nchini.
e) Kujadili makala maalumu za Kitaalamu zilizoandaliwa na Kamati Tendaji ya Taifa kuhusu maendeleo ya Nchi kwa ajili ya kuwasilisha kwenye mkutano mkuu wa Taifa.
f) Kutayarisha kanuni na masharti ya uendeshaji mzuri wa shughuli za Chama
g) Kutayarisha habari zote muhimu kwa ajili ya matumizi ya mkutano Mkuu wa Taifa
h) Wakati wa Chaguzi kwa nafasi za Serikali na za CCK kamati kuu ya Taifa itafanya kazi zifuatazo:-
i) Kupokea, kujadili na kupitisha majina ya wanachama watakao gombea nafasi za uongozi ngazi ya Taifa wa CCK kwenye Mkutano Mkuu wa Taifa
ii) Kupokea, kuchuja na kupitisha majina ya wanachama watakaogombea nafasi ya Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mgombea Urais wa Zanzibar pamoja na jina la mgombea Mwenza litakalowasilishwa na mgombea urais.

iii) Kuchagua wajumbe watano (5) watakaoingia kwenye kamati ya utendaji ya Taifa.

iv) Kuchagua Mweka Hazina, Katibu Mwenezi na Katibu Mipango na Uchumi wa CCK Taifa kutokana na mapendekezo ya Mwenyekiti wa CCK Taifa.

v) Kuteua wajumbe sita (6) wa Baraza la Wadhamini la CCK akiwemo na Mweka Hazina wa Taifa.

vi) Kuandaa Ilani ya Uchaguzi ya CCK na kutoa msukumo wa utekelezaji wa maamuzi na ahadi zilizotolewa na viongozi wa ngazi za juu wa CCK au vikao vinavyohusika

vii) Kufikisha maagizo na maazimio ya CCK mikoani na kutoa Uamuzi juu ya mapendekezo kutoka vikao vya CCK ngazi za chini na pia kuzipa miongozo kamati za utendaji za mikoa katika Mwenendo bora wa kukiimarisha chama na kuratibu shughuli za Kitaifa ili kuleta ufanisi zaidi.

viii) Kuandaa mkutano mkuu wa Taifa, kanuni na taratibu za shughuli za CCK kwa ngazi zote.

ix) Kushauri au kuandaa kamati ama tume kwa shughuli maalumu bila kuathiri majukumu ya kamati kuu ya Taifa na kurekebisha muundo wa CCK katika maeneo mbalimbali kadri itakavyoonekana inafaa kwa maslahi yake.

x) Kumuondoa madarakani kiongozi yeyote isipokuwa Mwenyekiti wa Taifa endepo utendaji wake wa kazi unamwondelea sifa za kuwa kiongozi na kiongozi aliyeondolewa madarakani anaweza kukata rufaa kwenye mkutano mkuu wa Taifa

xi) Kumuondoa madarakani kiongozi yeyote yule ambaye uteuzi au uchaguzi wake umefanywa na kamati kuu ya Taifa

xii) Kupanga makadirio ya mapato na matumizi ya CCK kwa mwaka

xiii) Kuandaa na kupitisha kanuni za fedha, ajira, uchaguzi, nidhamu, uongozi na vikao, pia kanuni za vitengo vya chama na kuruhusu kuanza kutumika.

xiv) Kumvua uanachama mwanachama yeyote isipokuwa Mwenyekiti wa Taifa iwapo itadhihirika kwamba amekiuka katiba maadili na nidhamu ya CCK aliyechukuliwa hatua hiyo anaweza kukata rufaa kwenye mkutano mkuu wa Taifa katika muda wa siku 14 tokea kupata taarifa ya uamuzi huo.

xv) Kusikiliza rufaa zote na malalamiko kutoka ngazi za Mkoa na Taifa na kuyatolea maamuzi ya haki

xvi) Kamati kuu ya Taifa ina mamlaka ya kumchagua makamu Mwenyeki Taifa bara au Zanzibar iwapo aliyechaguliwa na mkutano mkuu wa Taifa atakuwa amejiuzulu, amefukuzwa au amefariki dunia.

xvii) Kamati kuu ya Taifa ina uwezo wa kumrudishia uanachama mwanachama aliyefukuzwa na mkutano mkuu wa Taifa iwapo tu itaridhika na kutambua kwamba amejirekebisha.

xviii) Kamati kuu ya Taifa itafanya vikao vyake kila baada ya miezi mine yaani kwa mwaka mara tatu ila inaweza kukutana wakati wowote kwa Dharura endapo itaitishwa na Mwenyekiti wa Taifa kwa mashauriano na kukubaliana na Katibu Mkuu Taifa.

xix) Kamati kuu ya Taifa itakuwa na kazi ya kutunza nidhamu ya viongozi baada ya kupata taarifa toka kwenye kamati ya Nidhamu.

**3.8.6 Wajumbe wa Sekretarieti ya Taifa**

a. Mwenyekiti wa Taifa
b. Makamu wenyeviti Bara na Zanzibar

c. Katibu Mkuu
d. Naibu Katibu Zanzibar
e. Katibu Uenezi na Katibu Mipango na Uchumi
f. Mweka Hazina Taifa.
g. Katibu kiongozi ofisi ya katibu Mkuu na Naibu wake Zanzibar.

**3.8.7 Kazi ya Sekretarieti ya Taifa**

a. Kutakua na kamati ndogo ya kamati kuu ya Taifa itakayojulikana kama "Sekretarieti" ya Taifa ambayo itakuwa ndicho kiini cha uongozi na utendaji wa CCK.
b. Sekretarieti itafanya kazi zote za CCK kwa maelekezo ya Kamati Kuu Taifa.
c. Itasimamia shughuli za utendaji za kila siku ndani ya CCK
d. Sekretarieti ina uwezo wa kufanya kazi za kamati Kuu ya Taifa
e. Kuteua majina ya wagombea ubunge na uwakilishi endapo kamati Kuu ya Taifa haitaweza kukutana hivyo Sekretarieti itafanya kazi hiyo kwa niaba yake.

**3.8.8 Sekretariet itaunda Idara zitakazofanya kazi chini ya Katibu MkuuTaifa Idara hizo za Chama ni:**

a. Uhamasishaji , Kampeni na uchaguzi
b. Ulinzi na usalama
c. Mambo ya nje, ushirikiano wa Kimataifa
d. Fedha
e. Mipango na uchumi
f. Utafifi na sera

**3.8.9 Sekretarieti itateua wakuu wa Idara na vyuo kutokana na mapendekezo ya Mwenyekiti wa CCK Taifa.**

**3.8.10** Katibu Mkuu ataongoza vikao vya wakuu wa Idara na vyuo vyote vya CCK zitakazojumuisha Katibu Uenezi, Katibu Mipango na Mweka Hazina ngazi ya Taifa. Sekretarieti itafanya vikao vyake mara moja kila baada ya miezi mitatu, lakini inaweza ikakutana kwa Dharura.

**3.8.11 Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya Taifa**

i. Katibu Mkuu wa Taifa
ii. Katibu Kiongozi ofisi ya Katibu Mkuu
iii. Katibu mipango na Uchumi Taifa
iv. Katibu Uenezi Taifa
v. Mweka Hazina wa Taifa
vi. Wenyeviti na makatibu wa Vitengo vya Taifa
vii. Wakurugenzi wa idara za chama Taifa

**3.8.12 Kazi za Kamati ya Utendaji ya Taifa**

i. Kuandaa mikutano ya kamati kuu ya Taifa.
ii. Kusimamia utekelezaji wa shughuli zote za kila siku za chama
iii. Kulinda na kutunza siri za CCK
iv. Kuandaa mikakati na mbinu za kampeni za uchaguzi na nyinginezo.
v. Kamati ya utendaji inaweza kuunda kamati ndogo za CCK na kujiwekea utaratibu wake wa kufanya kazi kadri inavyoona inafaa kwa ajili ya kufanikisha shughuli za CCK

# SURA YA NNE

# UONGOZI WA KITAIFA

## VIONGOZI WAKUU NA WATENDAJI CCK

### 4.1. VIONGOZI WAKUU WA CHAMA

(a) Mwenyekii wa Taifa
(b) Makamu Mwenyekiti Bara na Zanzibar

**Watendaji Wakuu wafuatao.**

a. Katibu Mkuu Taifa.
b. Naibu Katibu Mkuu Zanzibar
c. Katibu Mkuu Kiongozi ofisi ya katibu Mkuu
d. Naibu katibu Mkuu kiongozi ofisi ya Katibu Zanzibar
e. Mhazini Taifa.
f. Naibu Mhazini Zanzibar
g. Katibu mipango na uchumi
h. Naibu katibu mipango na uchumi Zanzibar.
i. Katibu uenezi na Uhamasishaji sera.
j. Naibu Uenezi na uhamasishaji sera – Zanzibar.

4.1.1 Kazi za Mwenyekiti wa Taifa

a. Atakuwa ndiye Kiongozi Mkuu na pia ni Msemaji Mkuu wa CCK
b. Atakuwa ndiye Mhamasishaji Mkuu wa CCK na kiungo cha vikao vyote vya Kitaifa
c. Atakuwa ndiye Mwenyekiti wa Mkutano Mkuu wa Taifa na Kamati Kuu na Sekretarieti na Kamati ya Ulinzi na Usalama, utakapofika wakati wa uchaguzi wa viongozi wapya wa ngazi ya kitaifa atachaguliwa au kuteuliwa Mwenyekiti wa muda wa kuongoza kikao badala yake ambaye muda wake ulimalizika.
d. Atakua ndiye mlinzi wa katiba na mlinzi wa uhai wa CCK.
e. Ndiye atakayeitisha vikao vyote vya CCK ngazi ya kitaifa vya kawaida na vya dharura kwa mashauriano na katibu mkuu.
f. Atateua wajumbe watano (5) kuingia kwenye kamati kuu ya Taifa.
g. Atapendekeza majina yasiyozidi 25 ya wajumbe wa kuteuliwa kati ya hao ishirini wa kuingia kwenye mkutano mkuu wa Taifa baada ya kuidhinishwa na mkutano huo.
h. Atateua wajumbe wane (4) wa kamati ya ulinzi na usalama.
i. Anaweza kutengua uteuzi wa wajumbe wa kuteuliwa wa kamati ya ulinzi na usalama endapo utendaji wao hauridhishi
j. Atateua wajumbe sita wa kamati ya nidhamu ya Taifa
k. Atateua washauri katika maswala ya Siasa, Jamii na Uchumi
l. Atateua Mabalozi wa CCK watakaowakilisha chama chetu nchi za nje
m. Ataunda na kusimamia Kamati ya Muda kwa kadri ya umuhimu wa jambo lililopelekea kuundwa kwa kamati au tume hiyo. Kamati / Tume itakoma mara baada ya kuwasilisha taarifa ya kazi waliyopewa kufanya kwa Mwenyekiti wa Taifa
n. Katika mikutano ama vikao anavyoongoza zaidi ya kuwa na kura yake ya kawaida atakuwa pia na kura ya uamuzi (turufu) endapo kura za wajumbe wanaoafiki na wasio afiki zitalingana.
o. CCK kitakua na Wenyeviti katika ngazi zote kuanzia Shina hadi Taifa na watafanya kazi kama zilivyoanishwa ndani ya katiba hii isipokua hakutakuwa na nafasi za makamu wenyeviti shina hadi Mkoa

4.1.2 Kazi za Makamu Wenyeviti

a. Makamu Wenyeviti wa CCK Taifa ndio wasaidizi Wakuu wa Mwenyekiti wa CCK Taifa na watafanya kazi zote za chama watakazopewa na kuelekezwa na Mwenyekiti wa Taifa
b. Watahusika zaidi na shughuli za uhamasishaji na nyingine watakazopangiwa na Mwenyekiti Taifa
c. Watakua washauri wakuu wa Mwenyekiti Taifa na watafanya kazi zote watakazopewa toka ngazi za juu ya CCK.
d. Makamu Mwenyekiti Zanzibar ataimarisha Chama katika nyanja zote huko Zanzibar kwa maelekezo toka kwa Mwenyekiti Taifa.

4.1.3 Kazi za Katibu Mkuu wa CCK Taifa

a. Katibu Mkuu wa CCK atachaguliwa na Kamati Kuu ya Taifa kutokana na wajumbe wa kamati kuu ya Taifa kwa mapendekezo ya Mwenyekiti wa Taifa. Atakuwa kwenye madaraka kwa miaka mitano isipokuwa anaweza kuondolea na kikao kilichomchagua kushika nafasi hiyo
b. Atakuwa ndiye Mtendaji Mkuu wa CCK na atawajibika kwa shughuli zote za utendaji za chama.
c. Atafanya kazi zake kwa maelekezo ya Mwenyekiti wa Chama na Makamu Wenyeviti wa chama
d. Atawajibika kutunza Nyaraka zote na kuleta taarifa zake kama atakavyoelekezwa na Mwenyekiti wa Chama pia na vikao vya CCK ngazi ya Taifa.
e. Atawajibika kuandaa mikutano na vikao vyote vya ngazi ya Kitaifa kwa mujibu wa kalenda ya vikao na Katiba ya Chama.
f. Ataitisha na kuongoza vikao vya kawaida vya viongozi Watendaji Wakuu wa CCK kwa madhumuni ya kuandaa, kushauriana agenda za kamati kuu na kuchukua hatua za utekelezaji wa maamuzi ya chama.
g. Ataongoza na kuitisha kikao cha wakuu wa Idara na vyuo vya Chama kitakachokua na wajibu wa kuandaa agenda za Sekretarieti ya CCK Taifa
h. CCK kitakuwa na makatibu kuanzia ngazi ya shina hadi Taifa na watawajibika kufanya kazi hadi ngazi zao kama ilivyoanishwa ndani ya Katiba hii.

4.1.4 Kazi za Naibu Katibu Mkuu Zanzibar

Naibu Katibu Mkuu Zanzibar atachaguliwa na Kamati Kuu ya Taifa kwa mapendekezo yaliyowasilishwa na Mwenyekiti CCK Taifa.

a. Atakuwa ndio msaidizi mkuu wa Katibu Mkuu wa Chama na atafanyakazi zote za utendaji upande wa Zanzibar

4.1.5 Kazi za Katibu Kiongozi wa CCK Taifa.

a. Katibu Kiongozi atachaguliwa na kamati kuu ya Taifa kwa mapendekezo yaliyowasilishwa na mwenyekiti wa CCK Taifa, na atakuwa na naibu wake upande wa Zanzibar.
b. Pia atafanya kazi akiwa ni kiungo cha utekelezaji wa kazi za kila siku katika ofisi ya katibu mkuu na naibu katibu mkuu Zanzibar.
c. Atahusika na uwekaji mzuri wa nyaraka ambazo maamuzi yake tayari yameshatolewa na vikao vya Chama vya ngazi ya kitaifa na mikoa, pia kuhakikisha yanafanyiwa kazi ipasavyo.
d. Kuanzisha maswala ya kiutendaji kati ya taarifa za shughuli za CCK na za vitengo ambazo zitaandaliwa na kuzitolea taarifa kauli kwenye vikao vya kamati ya utendaji, kisha kuwasilisha kwenye kamati kuu ya Taifa.

e. Atakuwa ndiye katibu wa vikao vyote vya kamati ya utendaji na wakuu wa idara na vyuo vya CCK. Na ndiye muandaaji wa vikao hivyo baada ya kuitishwa na makatibu ama kwa mujibu wa kalenda.
f. Kuwa na mawasiliano ya karibu na makatibu wa mikoa kuhusiana na majukumu yao kiutendaji

4.1.6 Kazi za Katibu Uenezi wa Taifa

a. Kutakuwepo na Katibu Uenezi wa Taifa na Manaibu wake wawili (Bara na Zanzibar) ambao watachaguliwa na kamati kuu kwa mapendekezo ya Mwenyekiti Taifa
b. Kazi za Katibu Mwenezi Taifa na Manaibu wake ni kueneza sera, Ilani, Mikakati na mipango (programu) za CCK zilizokwisha amuliwa na vikao vya Chama.
c. Kusambaza taarifa mbalimbali za chama kadri atakavyopewa na viongozi wa Kitaifa na vikao vya chama.

4.1.7 Kazi za Katibu Mipango na Uchumi wa Taifa

a. Kutakuwepo na Katibu Mipango na Uchumi Taifa, na Manaibu wake wawili mmoja Bara na mmoja Zanzibar, atachaguliwa na Kamati Kuu kwa mapendekezo ya Mwenyekiti wa Taifa.
b. Kazi za Katibu Mipango Taifa ni kubuni na kuandaa mipango madhubuti ya kukipatia Chama mapato ya uhakika na endelevu kwa manufaa ya wanajamii sehemu walipo.
c. Atakua ndiye msimamizi mkuu wa mipango na uzalishaji katika chama na kusambaza mipango hiyo kwenye ngazi zote za chama Nchini.

4.1.8 Mhazini wa Taifa na Manaibu Wake.

a. Kutakuwepo na Mhazini wa Taifa na Manaibu wake wawili mmoja kwa upande wa Tanzania Bara na mwingine kwa upande wa Zanzibar, Mhazini Taifa na Manaibu wake watachaguliwa na Kamati Kuu ya CCK Taifa kutoka miongoni mwa wajumbe Kwa mapendekezo yatakayowasilishwa na Mwenyekiti wa Taifa.
b. Kazi za Mhazini Taifa :-
    i. Atakua ndiye Msimamizi Mkuu wa Idara ya fedha na mali za chama
    ii. Atatoa taarifa ya mapato na matumizi ya chama.
    iii. Ataandaa mapendekezo ya makisio ya mapato na matumizi ya kila mwaka ya chama na kuhakikisha yanakaguliwa na mkaguzi mkuu wa serikali na chama kupata hati safi
    iv. Atakua ni mjumbe wa Baraza la Wadhamini la CCK.

4.1.9 Kipindi cha Uongozi ndani ya CCK

a. Uongozi ndani ya chama ni miaka mitano (5) lakini mwanachama anaweza kuchaguliwa au kuteuliwa tena kuendelea na uongozi kwa vipindi vingine vya miaka mitano (5)
b. Kila kiongozi anapaswa kuhudhuria vikao vyote vya chama bila kukosa kiongozi ambaye atashindwa kuhudhuria vikao vitatu (3) mfululizo bila sababu atakuwa amejiondoa yeye mwenyewe kwenye uongozi, kipengele hiki kinazihusu ngazi zote za chama kuanzia ngazi za chini

# SURA YA TANO

## WAGOMBEA URAIS NA WAGOMBEA WENZA

### 5.1 WAGOMBEA URAIS NA WAGOMBEA WENZA

#### 5.1.1 MGOMBEA WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

a. Awe ametimiza masharti ya Katiba ya nchi kuhusu mgombea wa kiti cha Urais
b. Awe ni mwanachama wa CCK aliyetimiza sifa za kuwa kiongozi.
c. Aungwe mkono na wanachama wasiopungua mia mbili kwenye mikoa kumi (Minane Bara na Miwili Zanzibar) nchini
d. Awe anaielewa na kuitafasiri Katiba na Sera za CCK.
e. Atateua kwa kushirikiana na kamati kuu mwanachama Mwenye sifa zinzokubalika kichama kuwa mgombea mwenza wake wakati wa Kampeni na Urais ambaye atakuwa ni makamu wa Rais
f. Atachaguliwa na mkutano mkuu wa Taifa kwa mapendekezo ya kamati kuu ya CCK Taifa
g. Iwapo mgombea urais atashinda hivyo ndiye atakuwa mtunzaji na msimamizi wa Sera za CCK serikalini kwa uadilifu mkubwa
h. Isipokuwa kwa masharti ya ibara ndogoo ya 17.1 (e) ya Ibara hii, masharti haya hayatamhusu mgombea urais wa serikali ya mapinduzi ya Zanzibar kwa kuzingatia katiba ya Baraza la Mapinduzi Zanzibar.

#### 5.1.2 MGOMBEA WA SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR

a. Awe na vigezo vyote ambavyo vimemruhusu mgombea urais wa Muungano kichama
b. Atachaguliwa na mkutano mkuu wa Taifa wa CCK baada ya kupata mapendekezo ya Wajumbe wa mkutano mkuu toka Zanzibar, kwa kuzingatia Katiba ya Baraza la Mapinduzi Zanzibar.

#### 5.1.3 VIONGOZI WA KUU KUWA NA KOFIA MOJA.

(a) Haitaruhusiwa kwa Mwenyekiti, Makamu wote wa bara na Zanzibar, kuwania nafasi ya uraisi.
(b) Anaweza kufanya hivyo tu iwapo atawasilisha ombi lake kwenye mkutano mkuu na kisha kupata ridhaa ya yeye kufanya hivyo.
(c) Nafasi yake itajazwa iwapo katika mchakato wa kuwania nafasi ya uraisi au mwenza baada ya kipindi hicho na kwamba ameshinda.
(d) Iwapo hataweza kushinda ataendelea na nafasi yake katika uongozi alionao.
(e) Wanaweza kupata ruhusa ya kugombea ubunge au udiwani bila kuathiri nafasi zao.

## SURA YA SITA

## MENGINEYO

### 6.1 VITENGO VYA CHAMA CHA KIJAMII

CCK kitakua na vitengo vifuatavyo:-

6.1.1 Wanawake

(a) Wanawake wote wa CCK ambao ni wanachama hai watahusika na kuwa kwenye Kitengo
(b) Watawajibika kutengeneza kanuni za Kitengo chao na kuiwasilisha kwenye kikao cha kamati kuu ya CCK Taifa kwa kupitishwa.
(c) Kitengo cha wanawake kitakua chini ya uongozi wa Chama na Kitafuata Kalenda ya Vikao vya chama kuanzia ngazi zote bila ya kuathiri kanuni yao kwa kujiendesha kwa kuzingatia katiba ya CCK.
(d) Wakati ama kipindi cha uchaguzi au uteuzi wa nafasi za wagombea ubunge, udiwani kupitia viti maalum kitengo kitafuata ama kuzingatia taratibu zao walizojitungia wenyewe kwa mujibu wa Kanuni yao kisha majina yote ya wagombea yawasilishwe kwenye kamati kuu ya CCK Taifa kwa kuidhinisha uteuzi huo na si vinginevyo.
(e) Kitengo cha wanawake kitaundwa kuanzia kwenye mashina, vitongoji, Tawi, Kata, Wilaya, Mkoa na Taifa.

6.1.2 Kazi za kitengo cha wanawake:-

a) Kuwahamasisha wanawake kujiunga na CCK
b) Kuunda timu za wanawake kwa ajili ya kampeni za wagombea wa CCK kwenye nafasi za Serikali
c) Kuhamasisha na kuelimisha wanawake katika jamii kujiunga katika vikundi vya uzalishaji mali au huduma kwa lengo la kupunguza kero za wanajamii nchini kama ilivyoainishwa kwenye Katiba kuhusiana na Dira na Mwelekeo wa CCK.
d) Kuwahamasisha wanawake wajitokeze na kuthubutu kugombea Uongozi kwenye chaguzi za Chama na Serikali kwenye ngazi mbalimbali

6.1.3 Vijana

a) Kutaundwa kitengo cha vijana wa CCK nchi nzima kuanzia kwenye mashina, Vitongoji, Tawi, Kata, Wilaya, Mkoa na Taifa.
b) Sifa ni kuanzia Mwanachama mwenye umri wa miaka kumi na minane (18) hadi miaka arobaini (40) bila kujali jinsia au maumbile ana haki ya kuwa kwenye kitengo hiki cha vijana na kushika uongozi wa kuchaguliwa ama wa kuteuliwa.
c) Watawajibika kutengeneza kanuni ya Kitengo chao na kuwasilisha kwenye kikao cha kamati kuu ya CCK Taifa kwa kupitishwa
d) Kitengo kitakua chini ya uongozi wa CCK na kufuata kalenda ya vikao vya Chama kuanzia ngazi zote bila ya kuathiri kanuni yao kwa kujiendesha kwa kuzingatia mazingira ya CCK.

6.1.4 Kazi za kitengo cha Vijana

a) Vijana wa CCK ndio watakuwa chimbuko la kuanzishwa kwa vituo vya uzalishaji mali vya vijana.
b) Kueneza sera za CCK kupitia vijana wenzao ndani na nje ya Chama nchini kote.
c) Kuhamasisha vijana na wananchi kwa ujumla kujiunga na CCK.
d) Vijana wataunda mfumo Pathfinder wa CCK ambao ni vijana wenye umri ulio chini ya miaka kumi na minani nchi nzima kuanzia ngazi ya mashina ya CCK
e) Kubuni na kupanga mafunzo kwa vijana kuhusu masuala ya siasa, Uchumi na kijamii kwa mtiririko mahususi kuanzia ngazi za chini
f) Kuunda timu za vijana kwa ajili ya kufanikisha kampeni za wagombea wa CCK kipindi cha uchaguzi wa Kiserikali.

6.1.5 Kitengo cha Wazee.

a) Kutaundwa kitengo cha wazee miongoni mwa wanachama waliotimiza umri wa miaka zaidi ya hamsini na moja (51) kwa pamoja wataunda kitengo cha wazee wa CCK billa kujali jinsia na maumbile ya mtu.
b) Watawajibika kutengeneza kanuni za kitengo chao na kuwasilisha kwenye kamati kuu ya CCK Taifa kwa kupitishwa
c) Kitengo cha wazee kitakuwa chini ya uongozi wa Chama na kitafuata kalenda ya vikao vya chama kuanzia ngazi zote bila ya kuathiri kanuni yao kwa kujiendesha kwa kuzingatia katiba ya CCK
d) Kitengo cha wazee kitaundwa kuanzia kwenye Shina, Kitongoji Tawi Kata Wilaya, Mkoa na Taifa.

6.1.6 Kazi za kitengo cha Wazee

a) Kutoa ushauri kwa viongozi wa CCK katika ngazi zote na kuhakikisha kwamba sera za chama zinapewa msukumo mkubwa
b) Kuhakikisha kwamba haki za wazee na wastaafu wote zinalindwa baada ya kuzipigania kisheria na kuwanufaisha
c) Kuhamasisha wazee wenzao aidha wananchi kwa ujumla waweze kuwa wanachama wa CCK kwakujiunga na kitengo

6.1.7 Kitengo cha Wenye ulemavu

a) CCK kitakuwa na kitengo cha wenye ulemavu ambacho kitaundwa na walengwa kwa kuzingatia ulemavu wa mwanachama wa CCK.
b) Kitengo cha wenye ulemavu kitakuwa chini ya uongozi wa CCK kitafuata kalenda ya vikao vya chama kuanzia ngazi ya Kata, Wilaya, Mkoa na Taifa bila ya kuathiri kanuni yao kwa kujiendesha kwa kuzingatia katiba ya CCK
c) Watawajibika kutengeneza kanuni ya kitengo chao na kuwasilisha kwenye kamati kuu ya CCK Taifa kwa kupitishwa.

6.1.8 Kazi ya kitengo cha Wenye ulemavu

a) Kuratibu kero na matatizo yao na kupendekeza ni jinsi gani ya kuyatatua kwa kuyapatia ufumbuzi kwenye vikao vya chama husika na Kitaifa.
b) Kuhakikisha kuwa wanahamasisha wenye ulemavu na kuhamasika kugombea nafasi za uongozi katika chama na uongozi wa Kiserikali na kupata fursa sawa na wanachama wengine ndani ya CCK
c) Kupata takwimu sahihi ya idadi ya walemavu kutoka kila eneo la nchi kwa ushirikiano na uongozi wa CCK ngazi za shina, kitongoji Tawi na Kata hadi Taifa ili kutambua uwepo wao na mahitaji yao.

d) Kuhakikisha kwamba mali na misaada yote inayolenga kuwanifaisha wenye ulemavu kwa juhudi na uwajibikaji wa CCK kutoka kwa wafadhili inawafikia ipasavyo na kwa usimamizi wa viongozi wa kitengo na chama kwa pamoja ili kuepuka haki kutotendeka .
e) Kushawishi na kuwa na uwezo wa kuingiza wanachama kulingana na sera za CCK

6.1.9 Vitengo vitajuindia kanuni zao ambazo hazipingani na Katiba ya CCK. Hazitaanza kutumika mpaka zipate Kibali cha Kamati Kuu ya Chama Taifa.

6.1.10 Vitengo vyote katika ngazi zote vitakuwa vinafanya kazi zao chini ya uongozi wa CCK na vitafanya vikao vyao na kutoa taarifaa kwa uongozi wa Chama katika ngazi inayohusika ni jukumu la uongozi wa Chama katika kila ngazi kuhakikisha kuwa vitengo vinafanya kazi na kufanya mikutano yao kwa mujibu wa kanuni zao.

## 6.2 UTARATIBU WA KUCHAGUA WAGOMBEA NAFASI ZA UONGOZI.

6.2.1 Chini ya Katiba hii shughuli zote za uchaguli zitafanyika kwa kura ya siri au kura ya Wazi

6.2.2 Uchaguzi katika ngazi yoyote utafuata kanuzi za uchaguzi zilizopitishwa na kamati kuu ya Taifa

6.2.3 Maadili ya Uongozi:-

a) Kila kiongozi wa Kuchaguliwa au Kuteuliwa, atapaswa Kujiheshimu mara zote awapo ofisini au katika shughuli zake binafsi kwa ajili ya kudumisha mtazamo mzuri wa chama kwenye Jamii.

b) Kwa Kiongozi yeyote (Wa Kuchaguliwa au Kuteuliwa) atekaye kiuka maadili ya Chama yatakayo tolewa na Kanuni maalumu za Nidhamu za Kiongozi atachukuliwa hatua za kinidhamu kama Kanuni zitakavyoainisha.

c) Imekubalika na kuthibitishwa kwamba wanachama wanaoshika nafasi zote za uongozi wa kuchaguliwa au kuteuliwa watatimiza wajibu wao bila mshahara au malipo makuu ya kimkataba

d) Viongozi watakaoingia mkataba na CCK kama waajiriwa mikataba yao itaheshimiwa kwa kadri ya masharti na kanuni za chama.

e) Viongozi wote pamoja na wanachama wote kwa ujumla wao watawajibika kutafuta njia za kukiingizia chama mapato yake ili kuweza kujiimarisha na kuweza kulipa gharama za kukiwezesha Chama kuwepo ama kufanikisha kukidhi huduma au misaada katika jamii kwa kuzingatia Dira na mwelekeo wa CCK.

## 6.3 MALI NA FEDHA ZA CHAMA

6.3.1 Fedha zozote zitatokana na vyanzo mbalimbali vya CCK.

a. Fedha zozote zitakazolipwa kwenye Chama kwa njia ya michango ya hiari kutoka kwa Wanachama.
b. Fedha zozote zitakazopatikana kwa njia ya kiingilio na ada ya mwaka kutoka kwa wanachama.
c. Faida itakayopatikana kutoka katika miradi ya Chama
d. Fedha zozote ambazo zitalipwa kisheria kwa chama kama matokeo ya Kampeni ya uchaguzi kwa uhamasishaji pamoja na michango ya wahisani uenezi na njia nyinginezo za kiuchumi zinazoendeshwa na Vyombo vya Chama

e. Fedha zozote au mali zitakazolipwa kwa chama kwa ajili ya michango ruzuku, zawadi , mikopo na mali za Urithi
f. Fedha zitakazotokana na riba kutoka benki na taasisi za fedha.

6.3.2 Usimamizi wa mali na fedha za CCK

a. Fedha zote za Chama zitakusanywa au kupokelewa kwa stakabadhi ya Chama
b. Fedha zote za chama zitahifadhiwa katika Benki teule au mabenki Mengine kama Kamati Kuu ya CCK itakavyoamua kufuatana na sheria za ndani za fedha za CCK.
c. Mhazini atahakikisha kwamba akaunti zote zilizo benki zitakua kwa jina la chama cha CCK na zitaendeshwa kwa kuzingatia kanuni na masharti yaliyowekwa na Chama.

## 6.4 NAFASI ZIKIWA WAZI

Nafasi ya uongozi ikiwa wazi kwa sababu yeyote ile kamati kuu ya Taifa itaandaa utaratibu wa kujaza nafasi hiyo mara moja na kwamba nafasi hiyo iliyo wazi haitafanya shughuli za Chama zisizotendeka ila pale tu katiba hii inapoelekeza vinginevyo aidha kamati za ngazi ya chini zitafanya hivyo.

## 6.5 BARAZA LA WADHAMINI

6.5.1 Kutakuwepo na Baraza la wadhamini la CCK ambalo litaundwa na idadi ya wajumbe sita (6).

6.5.2 Wajumbe wa Baraza la wadhamini

a. Mwenyekiti wa Baraza
b. Katibu wa Baraza
c. Wajumbe (wanne ) wa Baraza

6.5.3 Wajumbe wa Baraza la wadhamini watateuliwa ama kuchaguliwa na kamati kuu ya Taifa baada ya majina yao kupendekezwa na Mwenyekiti wa Taifa wa CKK na miongoni mwao pawe na mjumbe au wajumbe wa Baraza kutoka Zanzibar watakuwa na wadhifa huo kwa kipindi cha miaka mitano (5) na mjumbe anaweza kuteuliwa au kuchaguliwa tena baada ya muda wake kumalizika.

6.5.4 Kazi na mamlaka ya Baraza la Wadhamini

a. Kuweka chini ya uangalizi wake mali zote za chama zinazoondosheka na zisizoondosheka, itaheshimu sheria na taratibu zilizowekwa na sheria ya Nchi inayohusu wadhamini
b. Baraza litafanya kazi zake chini ya usimamizi na maelekezo ya kamati kuu ya Taifa.
c. Kuingia katika shughuli zozote za uchumi ambazo zinaendana na madhumuni na malengo ya CCK kwa kibali cha kamati kuu ya Taifa
d. Kuunda kamati ndogo ndogo na kukasimu kwa kamati hizo madaraka yake ya utendaji na utekelezaji wa shughuli zake
e. Bila ya kuathiri masharti ya sheria na kanuni ya Baraza la Wadhamini Baraza linaweza kuitisha mkutano maalum wa Kamati Kuu ya Taifa pale itakapolazimu kufanya hivyo.

f. Wajumbe wa Baraza la wadhamini watamteua Mwenyekiti wao miongozi mwao, na Katibu wa Baraza la wadhamini.

6.5.5 Kukoma au kuondolewa kwa mdhamini

a. Ikiwa ana afya mbaya kiasi cha kushindwa kufanyakazi zake
b. Ameonesha uwezo mdogo katika kutekeleza majukumu yake.
c. Kama atakua amekiuka katiba na maadili ya CCK.
d. Kama atapatikana na hatia ya Kosa ambalo kamati kuu Taifa itaridhika kuwa halikustahiki kufanywa na mdhamini wa Chama
e. Kama atafariki
f. Kama atafirisiwa na kushindwa kujikomboa katika kipindi cha miezi sita (6).
g. Mdhamini atajiuzulu kutoka katika Baraza kwa kutoa tamko la maandishi kwa kamati kuu ya Taifa kupitia kwa Mwenyekiti wa Baraza
h. Kama itatokea nafasi kuwa wazi kutokana na kifo, kujiuzulu au kufukuzwa kwa mdahamini nafasi hiyo itajazwa mara moja kufuatana na taratibu za Katiba hii na sheria inayotunika.
i. Kama mwenyekiti wa Baraza atashindwa kuhudhuria kikao au vikao wajumbe watamteua Mmojawapo kati yao kuwa Mwenyekiti wa kikao cha siku hiyo.
j. Mwenyekiti wa Baraza atakuwa na haki ya kutumia kura yake ya turufu mbali na ile ya kawaida kuamua pindi kura za wajumbe zikifungana

## 6.6 MAAMUZI YA VIKAO VYA CCK

6.6.1 Akidi ( Quarum)

Akidi katika vikao vya Chama itakuwa ni zaidi ya nusu ya wajumbe wote wanaostahili na kupaswa kuhudhuria kikao

6.6.2 Maamuzi

a. Kwa kawaida maamuzi yatafikiwa kwa kauli ya maafikiano (Consensus) lakini itakapolazimika kura zitapigwa ili kufikia ama kupata maamuzi
b. Maamuzi yote isipokuwa ilipoelekezwa vinginevyo katika Katiba hii yataafikiwa kwa zaidi ya nusu ya wajumbe waliohudhuria na kupiga kura
c. Mwenyekiti wa kikao atakuwa na kura ya maamuzi zaidi ya kura yake ya kawaida
d. Maamuzi ya kubadilisha Katiba yatafikiwa kwa theluthi mbili $^{2}/_{3}$ ya kura zote za wajumbe waliohudhuria na kupiga kura.
e. Maamuzi ya kumwondoa Mwenyekiti yatafikiwa na theluthi mbili ya wajumbe wote wanaostahili kuhudhuria kikao cha mkuatano Mkuu wa Taifa.

6.6.3 Kuheshimu maamuzi

a. Mwanachama ama kiongozi yoyote anao wajibu wa kuheshimu maamuzi yaliyofanywa na vikao vya Chama.
b. Kutokuheshimu maamuzi ya vikao vya chama nikuvunja Katiba hii
c. Kiongozi au mwanachama yeyote ambaye haridhiki na maamuzi ama Uamuzi wowote uliofikiwa na kikao chochote cha chama anaweza kukata rufaa kwenye kikao cha juu zaidi cha Chama na atakuwa na haki ya kusikilizwa.
d. Kulalamikia maamuzi ya Chama nje ya Vikao vya chama ni kuvunja maadili ya kanuni na Katiba ya CCK

## 6.7 TAASISI NA NAFASI NYINGINE ZA CCK

6.7.1 Kutakuwa na Taasisi za Chama kama ifuatavyo:-

i. Vyuo vya Chama
ii. Kampuni za uchumi za Chama
iii. Vyombo vya habari vya chama

6.7.2 Kamati kuu ya Taifa itaunda taasisi zilizoorodheshwa katika Ibara hii na itakuwa na mamlaka ya kuunda taasisi nyingine yoyote ambayo haijaorodheshwa katika Ibara ndogo ya 4.1 kama itakavyoona inafaa kwa maslahi na maendeleo ya CCK.

6.7.3 Makamisaa wa Chama

i. Makamisaa wa Chama ni makada maalumu watakaoteuliwa na kamati kuu kila itakapoona inafaa kutekeleza majukumu maalumu ya kisiasa na kiutendaji
ii. Kamati kuu ya Taifa itakuwa na mamlaka ya kuunda nafasi na kuteua mwanachama kuishika nafasi hiyo kwa maslahi na maendeleo ya CCK na wanajamii kwa ujumla.

6.7.4 Kamati maalum ya kamati kuu Zanzibar

i. Itakuwa ni sehemu ya kamati kuu ya Taifa
ii. Itafanya kazi yake kwa maelekezo ya kamati kuu Taifa
iii. Itawajibika kwa kamati kuu ya Taifa
iv. Itafanya kazi yake katika eneo la Tanzania Zanzibar.
v. Kamati ya utendaji ya Kamati kuu Zanzibar itafanya Vikao vyake mara moja kila baada miezi minne au inaweza kukatana kwa Dharura inapobidi kufanya hivyo.

6.7.5 Wajumbe wa kamati maalum ya kamati kuu Zanzibar

a. Makam mwenyekiti Zanzibar
b. Naibu Katibu Mkuu Zanzibar
c. Wajumbe wa Kamati kuu toka Zanzibar
d. Wenyeviti na Makatibu wa vitengo vya Chama Taifa kama watatoka Zanzibar
e. Wenyeviti wa Wabunge na wawakilishi waliochaguliwa kwa tiketi ya CCK katika Zanzibar
f. Makatibu wa CCK wa Mikoa ya Tanzania Zanzibar
g. Naibu mweka Hazina Zanzibar
h. Naibu katibu Uenezi Zanzibar
i. Naibu Katibu mipango Zanzibar
j. Wenyeviti wa mikoa ya Zanzibar
k. Wakuu wa Idara na vyuo vya CCK vilivyopo Zanzibar
l. Naibu Katibu Kiongozi ofisi ya Naibu Katibu Mkuu Zanzibar

6.7.8 Kazi za kamati ya Maalum ya kamati kuu Zanzibar

a. Kuunda Sekretarieti chini ya Naibu Katibu Mkuu Zanzibar na kuipa majukumu kwa namna itakavyoona inafaa kwa Zanzibar
b. Kumchagua ama kumteua Katibu wa kamati ya utendaji ya kamati kuu Zanzibar
c. Kumchagua mweka Hazina

d. Kupanga Shughuli za Chama katika Zanzibar
e. Kutekeleza sera za chama kama zilivyopitishwa na mkutano mkuu wa Taifa
f. Kuweka ufuatiliaji wa kutosha Mkoa hadi Mkoa na kuhakikisha kwamba kazi za CCK zinatekelezwa kikamilifu na kuwa na matokeo yaliyokusudiliwa
g. Kutathimini utekelezaji wa shughuli zote za Chama katika Zanzibar
h. Kubuni, kujenga na kudumisha uhusiano mwema kati ya Chama na wananchi na kuwaelimisha juu ya sera, malengo na mwelekeo pamoja na Dira ya CCK
i. Kujadili na kutoa maoni kwa kamati kuu Taifa juu ya wanachama wanaomba kugombea urais wa Serikali wa Mpinduzi ya Zanzibar.
j. Inaweza kumsimaisha uongozi kiongozi yoyote kwa Zanzibar

**Wajumbe wa kamati ya utendaji ya kamati maalum Zanzibar.**

a. Naibu katibu Mkuu Zanzibar
b. Katibu aliyeteuliwa na kamati maalum Zanzibar.
c. Naibu katibu mwenezi
d. Naibu katibu mipango
e. Naibu mweka Hazina
f. Wenyeviti na makatibu wa vitengo vya chama ngazi ya Taifa Zanzibar
g. Wakuu wa idara na vyuo vya CCK Zanzibar
h. Naibu Katibu Kiongozi ofisi ya naibu Katibu Mkuu Zanzibar

6.7.9 Kamati ya Ulinzi na usalama ya CCK

a. Kutakua na kamati ya ulinzi na usalama ya Chama ambayo itaongozwa na Mwenyekiti wa CCK Taifa.

6.7.10 Wajumbe wa kamati ya ulinzi na usalama Taifa

a. Mwenyekiti wa Chama
b. Makamu Mwenyeviti wa Chama Bara na Zanzibar
c. Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu Bara na Zanzibar
d. Wajumbe wanne wa kuteuliwa na Mwenyekiti mmoja wao atoke Zanzibar
e. Rais wa Jamhuri ya Muungano kama atatoka CCK
f. Waziri mkuu iwapo atatoka CCK
g. Rais na makamu wa kwanza wa Rais Zanzibar kama atatoka CCK

6.7.11 Kazi za kamati ya ulinzi na usalama

a. Kuhakikisha kwamba usalama wa Chama na viongozi wa CCK unakuwepo Nchini kote
b. Kukikinga chama kutokana na njama za ndani na nje ya chama
c. Kuhakikisha usalama wa mali za chama unakuwepo.
d. Wajumbe wa kamati wanaotoka Zanzibar watashughulika zaidi na upande wa Zanzibar
e. Kuratibu mwenendo wa Utendaji wa vijana kama walinzi wa CCK

6.7.12 Uongozi wa kamati ya ulinzi na usalama.

Kutakuwa na Katibu wa kamati ya Ulinzi na usalama ya CCK atakayeteuliwa na Mwenyekiti waTaifa baada ya kushauriana na makamu Wenyeviti, Naibu Katibu Mkuu wa upande wa Zanzibar atakuwa Katibu wa kamati hiyo kwa Tanzania Zanzibar.

6.7.13 Kazi za Katibu wa kamati ya ulinzi na usalama.

a. Ndiye atakaekuwa Katibu wa vikao vyote vya kamati hiyo.
b. Atatekeleza kazi zote atakazopewa na kamati hiyo au na Mwenyekiti wa chama
c. Atakuwa msimamizi mkuu wa shughuli zote za walinzi wa CCK
d. Ataitisha vikao vya kamati kila mara itakapolazimu akiongozwa na Mwenyekiti
e. Kwa Zanzibar kazi za katibu wa kamati zitafanywa na Naibu Katibu Mkuu Zanzibar.

6.7.14 Wajumbe wa kamati za ulinzi na usalama kuanzia shina hadi Mkoa

a. Wenyeviti wa Chama kwa ngazi inayohusika
b. Makatibu wa Chama kwa ngazi inayohusika
c. Wajumbe watatu (3) wa kuteuliwa na Mwenyekiti wa ngazi husika
d. Mkuu wa Mkoa, Wilaya , Kata na Afisa Mtendaji pia Kijiji aliyetoka CCK

6.7.15 Makatibu wa CCK kuanzia Tawi hadi Mkoa

watafanya kazi zao kama zilivyoainishwa kwenye wajibu wao kwa mujibu wa katiba hii

6.7.16 Kamati ya nidhamu ya Chama ya Taifa

a. Kutakuwa na kamati ya Nidhamu ya CCK Taifa ambayo Mwenyekiti wake pamoja na wajumbe watateuliwa na Mwenyekiti Taifa
b. Kamati za nidhamu zitaundwa katika ngazi zote za chama kufuata muundo wa kitaifa
c. Mwenyekiti wa Taifa anaweza kutengua uteuzi wa mjumbe yeyote wa kamati ya Nidhamu iwapo itaonekaa kwamba utendaji wake wa kazi hauridhishi

6.7.17 Wajumbe wa kamati ya nidhamu ya CCK

a. Katibu mkuu wa chama Taifa
b. Manaibu katibu Mkuu
c. Wajumbe watatu (3) wa kuteuliwa na Mwenyekiti mmoja wao atoke Zanzibar
d. Kamati itakutana mara moja kwa mwezi lakini inaweza kuitishwa kwa dharura wakati wowote.

6.7.18 Kazi za kamati ya Nidhamu ya CCK

a. Kuhakikisha nidhamu inakuwepo ndani ya CCK
b. Kusimamia maadili ya viongozi wa Kitaifa na Mikoa na kutoa mapendekezo kwenye vikao vya kamati kuu yaTaifa kwa hatua zaidi
c. Kuhakikisha viongozi na wanachama wote kwa pamoja wanaheshimu katiba na inafuatwa ili kujenga nidhamu ya kweli kwa misingi mikuu ya UPENDO, HESHIMA NA MSHIKAMANO.

## 6.8 MAREKEBISHO YA KATIBA YA CCK.

Katiba inaweza kurekebishwa na kupitishwa na mkutano mkuu wa Taifa kutokana na mapendekezo ya Kamati kuu ya Taifa yatakayoungwa mkono na theluthi mbili ya wajumbe wa mkutano Mkuu wa Taifa wenye haki ya kupiga kura.

6.8.1 Ushirikiano wa vyama kisiasa

CCK itadumisha ushirikiano na chama chochote cha siasa hapa Nchini na Duniani kwa malengo ya kudumisha udugu kati ya jamii za Watanzania kwa amani na utulivu duniani.

## 6.9 KUVUNJA CHAMA

CHAMA CHA KIJAMII hakitajifuta kamwe kwa faida ya kikundi chochote.

CCK

Matumaini mapya Kwa Watanzania

- Dumisha umoja na Uzalendo
- Pambana na RUSHWA NA UFISADI
- Mabadiliko ni sasa, mabadiliko ni sisi

***************************************************************************